# Nipashe

Jumamosi Septemba 14, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581799

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


**Mwalimu** mbaroni madai ya kulawiti mwanafunzi akiwa masomo ya ziada

UKURASA 3

**Serikali** kuwapima watumishi waraibu wa dawa za kulevya

UKURASA 4

**Waziri** asisitiza mchakato kuhama hiari Ngorongoro bado uko palepale

UKURASA 4



TEN HAG AMJIBU CRISTIANO RONALDO

UKURASA 22



# Polisi yapiga marufuku maandamano CHADEMA

• **Yenyewe** yatoa kauli kwamba yatakuwapo kama ilivyopangwa ... *Uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 17

### TRUMP AKATAA MDAHALO MWINGINE NA KAMALA



MGOMBEA wa chama cha Republican, Donald Trump, amekataa kushiriki mdahalo mwingine na Kamala Harris, wa chama cha Democrat kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu Novemba 5, mwaka huu...

## Waziri Biteko atangaza neema kushuka bei ya nishati kupikia

UKURASA 3




Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emannuel Nchimbi akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari, katika Ofisi ndogo za Makao Makuu ya CCM, Lumumba, jijini Dar es Salaam jana, alipokuwa akijibu hoja mbalimbali kutokana na matukio ya kutekwa na kuuawa kwa watu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## CCM yaunga mkono uchunguzi wa matukio utekaji, mauaji ya raia

UK. 2

**MICHEZO** GAMONDI ATAMBA KUONESHA UKUBWA UK.24

**MAONI,** UK.6



Mafundi wa mkandarasi wakiendelea na ujenzi kituo cha mabasi yaendayo haraka katika eneo la Posta Mpya, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Polisi yapiga marufuku maandamano CHADEMA

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Jeshi la Polisi likionya maandamano yaliyopangwa na viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuwa atakayeshiriki atakabiliwa vilivyo, wenyewe wamelitunishia 'misuli' jeshi hilo kwa kueleza kuwa ratiba iko pale pale.

Jana, Jeshi la Polisi kupitia Msemaji wake, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, lilionya yeyote atakayeingia barabarani atakabiliwa vilivyo.

Kauli hiyo imetolewa baada ya chama hicho siku mbili zilizopita kuwaita makada wake kutoka mikoa mbalimbali kwenda Dar es Salaam kushiriki maandamano.

CHADEMA imetangaza kuanzia Septemba 23, mwaka huu, wataanza kuingia barabarani kushinikiza viongozi kadhaa kujiuzulu kutokana na mauaji ya Mjumbe wa Sekretarieti ya chama hicho, Ally Kibao.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika Shule ya Polisi Tanzania (TPS), Moshi, mkoani Kilimanjaro, DCP Misime alionya chama hicho kuacha kuendelea kuhamasisha wananchi kujihusisha katika uhalifu huo na atakayeingia barabarani atakabiliwa vilivyo kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Hatua hiyo waliyofikia (CHADEMA) tunajiuliza na tunaendelea kufuatilia na uchunguzi kwa nini wanataka kututoa kwenye reli ya hatua za kiupelelezi zinazoendelea, baada ya Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Samia Suluhu Hassan, kuelekeza au kuagiza vyombo vifanye uchunguzi kisha kuwasilisha taarifa kwake," alisema DCP Misime.

Alisema mara kadhaa viongozi na wafuasi wa chama hicho wamekuwa wakipanga, kuratibu mikakati mbalimbali na kutoa matamshi yenye lengo la kutaka au la kuleta vurugu nchini, ili kuharibu amani ya nchi kwa sababu wanazozijua wao wenyewe.

DCP Misime alisema Jeshi la Polisi linatoa onyo kwa viongozi wa chama hicho, kuacha kuendelea kuhamasisha wananchi kujihusisha katika uhalifu huo, na yeyote atakayeingia barabarani atakabiliwa vilivyo kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Kwa maana hiyo, maandamano hayo yamepigwa marufuku. Jeshi la Polisi linatoa katazo kwa yeyote aliyealikwa, kuelekezwa kufika Dar es Salaam kutoka mkoa wowote ule kwa ajili ya maandamano hayo asithubutu kufanya hivyo, kwani maandamano hayo ni haramu na hayatafanyika.

"Hivyo asipoteze muda na gharama yake. Jeshi la Polisi Nchini, linaendelea kutoa rai kwa wananchi wapenda amani kutokubali kurubuniwa, kudanganywa au kushawishiwa kwa namna yeyote ile kushiriki katika maandamano hayo na badala yake waendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi kutoa taarifa za viashiria vyovyote vya uvunjifu wa amani," alisema.

**CHADEMA YAJIBU**

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alipoulizwa na Nipashe kuhusu onyo hilo, alisema msimamo wao ni kwamba,maandamano yaliyopangwa yako palepale.

"Tutatoa ratiba wapi yanaanzia na kuishia. Msemaji wa Polisi si mamlaka halali ya kuzuia maandamano yetu. Sheria inamtambua Mkuu wa Polisi Wilaya husika na sisi tutafuata sheria kuliarifu Jeshi la Polisi kwa sababu mpaka sasa hatujaliarifu maandaamano yetu yataanzia wapi na kwenda wapi," alisema.

Mrema alisema mpaka Septemba 21, mwaka huu, endapo watakuwa hawajawaachia watataarifu rasmi maandamano hayo.

"Kauli ya msemaji wa Jeshi la Polisi tunaichukulia kama kauli nyingine lakini kwa mujibu wa sheria hana mamlaka ambayo amejipa kwa mujibu wa sheria yenyewe ya Jeshi la Polisi lenyewe," alidai.

Septemba 11, mwaka huu, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akiwa Mikocheni mkoani Dar es Salaam, ikiwa ni siku chache baada ya maziko ya Kibao alinukuliwa akisema:

"Nimetangaza hadi kufikia Septemba 21, mwaka huu, tunategemea tuone hatua za watu kuwajibika kuwarejesha waliotekwa na viongozi kadhaa kujiuzulu.

"Kama hawatochukuliana hatua wenyewe kwa wenyewe sisi kuanzia Septemba 23, 2024 jiji lote la Dar es Salaam kila kata kila mtaa, wawe tayari.

"Ndugu zangu tumekuwa tunafanya utani mara nyingi 'this time around' hatuna utani, kuanzia Jumatatu Septemba 23, mwaka huu, sisi tutaingia barabarani kudai uhai wa watu wetu waliopotezwa 'unless' serikali ichukue hatua za haraka na za makusudi kuwarejesha watu, kujiuzulu na watu wote kuwajibika," alisema.

Aidha, Mbowe alisema kabla ya maandamano hayo Kamati Kuu ya CHADEMA itakutana Septemba 16 na 17, kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ikiwamo utekaji, mauaji na kupotea kwa viongozi wao.

**•Imeandikwa na Godfrey Mushi (MOSHI) na Romana Mallya (DAR)**

# CCM yaunga mkono uchunguzi utekaji, mauaji

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetoa taarifa rasmi kuhusu matukio ya utekaji na mauaji ya raia huku kikisema kinaunga mkono maagizo ya kufanyika kwa uchunguzi na watuhumiwa wafikishwe katika vyombo vya sheria.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza kufanyika kwa uchunguzi dhidi ya matukio hayo baada ya kutekwa na hatimaye kuuawa kwa aliyekuwa kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ally Kibao, na mwili wake kukutwa katika eneo la Ununio, Dar es Salaam, ukiwa umeharibika.

Kutokana na kifo hicho, kumekuwa na kauli mbalimbali kutoka kwa viongozi wa vyama vya siasa, mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao Tanzania, wanasheria na makundi mbalimbali kutaka uchunguzi wa kina ufanyike huku baadhi wakishauri vyombo vya usalama vya ndani visifanye kazi hiyo kwa kuwa vinatuhumiwa kuhusika.

Wengine wameshauri kuundwa kwa tume ya kijaji ya uchunguzi wa matukio hayo kwa kuwa itakuwa huru na wengine wakitaka vyombo vya nje kama Scotland Yard kufanya jambo hilo.

Katibu Mkuu wa CCM, Blozi Dk. Emmanuel Nchimbi, akizungumza na wahariri na waandishi waandamizi wa vyombo vya habari jana, jijini Dar es Salaam, alisema chama kinaunga mkono kufanyika kwa uchunguzi wa matukio hayo ambayo yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara.

Dk. Nchimbi alisema suala la kudumisha umoja na mshikamano limo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020- 2025 na kwamba inaunga mkono kauli ya Rais Samia ya kufanyika kwa uchunguzi kuhusu matukio hayo na watuhumiwa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Kifungu cha 105 cha Ilani ya CCM kinasema: "Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhimiza serikali zake kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu, raia wake na mali zao ili kudumisha umoja, mshikamano, amani na utulivu ambazo ni tunu kuu za taifa letu," alisema Nchimbi huku akinukuu kifungu hicho.

"Mtu yeyote atakayehatarisha, kushiriki kuteka raia, mauaji ya raia au kikundi chochote kitakachofanya hivyo ili kuharibu taswira ya CCM, hicho hakina nia nzuri na CCM bali kitakuwa na lengo la kuichonganisha CCM na wananchi. CCM si ya watu wajinga, watekaji na wauaji. CCM ni chama cha siasa kinachojitambua na kama kuna chama cha siasa kinafanya hivyo basi ni chama kisichojitambua," alisema.

Pamoja na kusisitiza kuwa chama kinaunga mkono kufanyika kwa uchunguzi huo, Dk. Nchimbi alisema hatua hiyo isiwe ya kukomoana au kulipizana visasi bali haki itendeke. Alisema watu watakaotuhumiwa kuhusika na vitendo hivyo, wapewe nafasi ya kujitetea kwa mujibu wa sheria na mtu asionekane kuwa mkosaji hadi atakapothibitika kupitia mahakama.

**AWATETEA MBOWE, MNYIKA**

Dk. Nchimbi alisema kumekuwa na tuhuma kwamba Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na Katibu Mkuu, John Mnyika, wanahusika na matukio hayo jambo ambalo haamini na lina mtazamo wa kukomoana kisiasa.

"Siku ya tukio la kupatikana kwa mwili wa Kibao, Mbowe alinipigia simu mara tano lakini sikupokea. Baadaye nilimwandikia ujumbe mfupi kwa njia ya simu (sms). Nilipokutana naye nilimwomba msamaha na alionesha wazi sura yake si ya utekaji na alichokuwa akikisema alikuwa anamaanisha.

"Mbowe si mtekaji wala Mnyika. Mnyika jinsi alivyo unamtuhumu kuwa mtekaji? Akiona hata panya anakimbia. Sasa huyo anaweza kuwa mtekaji au muuaji?" alihoji Dk. Nchimbi.

Sambamba na hayo, kutokana na kuwapo kwa utekaji na mauaji ya raia, kumekuwa na jitihada za kuwafarakanisha polisi na raia jambo ambalo halina mustakabali mzuri kwa taifa. Alisema jambo hilo linapaswa kukemewa na viongozi wa siasa na wananchi kwa ujumla.

"Sisi ambao tunakwenda huko hadi vijijini tunajua uhusiano mzuri uliopo kati ya wananchi na polisi. Baadhi ya maeneo wananchi wanajenga vituo vya polisi na sehemu zingine wanafikia hatua na kuomba serikali imalizie. Yote hiyo ni kuonesha umuhimu wa Jeshi la Polisi kwa usalama wa raia na mali zao.

"Hapa Dar es Salaam iliwahi kutokea watu wakadai kwamba trafiki ni chanzo cha foleni barabarani. RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa) wakati ule aliwaambia polisi watoke barabarani. Kilichotokea ni kwamba kulikuwa na foleni za ajabu Dar es Salaam nzima. Tuache maneno ya kuwachonganisha polisi na wananchi," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Nchimbi alisema CCM bado inaamini katika mazungumzo na kwamba ndiyo njia pekee ya kujenga nchi kwa vyama vya siasa kukutana na kuzungumzia masuala mbalimbali kwa mustakabali wa nchi na ustawi wa demokrasia.

Alisema kwa kutambua hilo, kuna mchakato wa kurejesha mazungumzo baina ya vyama vya siasa kwa kuwa anaamini kupitia jambo hilo ndipo maelewano yatakapopatikana na watu kuishi kwa amani na upendo bila kujali itikadi zao za kisiasa.

HABARI KITAIFA

# Mzazi aanika risasi ilivyoua mwanafunzi

**Na Vitus Audax**

RISASI iliyosababisha kifo cha mwanafunzi wa Kidato cha Nne katika Shule ya Sekondari ya Lulembele, Teresia John (18), ambaye alifariki dunia wakati wa vurugu na maandamano ya wananchi katika Kituo cha Polisi Lulembela, wilayani Mbogwe, mkoani Geita, ilipitia dirishani, imeelezwa.

Mama mzazi wa mtoto huyo, Grace Wilson, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari waliofika nyumbani kwake kufuatilia tukio hilo.

Mauaji hayo yalitokea Jumatano ya wiki hii wakati wananchi wakitaka kuwashambulia na kuwaua watu wawili waliotuhumiwa kuiba mtoto.

Grace alisema risasi hiyo ilipitia dirishani na kupasua kioo kisha kumpata mtoto wake aliyekuwa chumbani muda mfupi baada ya kuwataka waingie ndani kuepuka vurugu hizo.

"Alikuwa chumbani nilishtuka anakuja anakimbia sebuleni tulipokuwa sisi, alifika akaniangukia kifuani na kupoteza maisha hapo hapo. Nivyomwangalia kifuani damu zilikuwa zinatoka, niliona tundu limetokea mgongoni," alisimulia mama huyo.

Grace kabla ya tukio hilo mtoto wake, alikwenda kwa fundi kujaribisha nguo aliyotakiwa kuivaa katika sherehe ya dini. Aliporudi vurugu zilikuwa zimeanza, hivyo akatutaka tuingie ndani na yeye akaingia chumbani ambako tukio hilo lilimkuta.

**MTENDAJI AFUNGUKA**

Mtendaji wa Kata ya Lulembela, Frank Gonja, alisema wakati tukio hilo linatokea kulikuwa na gulio na watu walikuwa wengi.

"Baada ya kuwaona vijana hao waliobeba watoto, mmoja akiwa hana nguo walianza kushambuliwa. Hisia ziliwatuma kuwa ni miongoni mwa matukio ya wizi wa watoto, hivyo hawakutaka kujiridhisha, wakaamua kuwashambulia, walikuwapo watendaji wa vijiji, lakini walipotaka kusaidia hali ilikuwa mbaya zaidi," alisema Gonja.

Alisema alipokea taarifa kuwapo kwa vurugu hizo, hivyo kuelekea katika eneo la tukio akiwa na pikipiki ambako alifanikiwa kuwabeba vijana hao ambao walikuwa na watoto na kuwapeleka katika kituo cha polisi ambako pia wananchi waliwafuatilia nyuma.

Baada ya kuwafikisha kituoni, alisema waliwahoji na kubaini kuwa watoto wale ni wa mmoja wao na walijihakikishia kwa kuwasiliana kwa simu na mama yake ambaye alithibitisha kwa majina ya watoto hao kisha kufika kituoni na watoto kumtambua.

"Wananchi walijulishwa lakini hata hivyo hawakutaka kuelewa na kuendelea na vurugu na ndipo walipoomba msaada wa askari kutoka wilayani na mkoani, ambao walisaidia kutuliza vurugu hizo na ikatambulika kuwa kuna watu wawili wamefariki dunia," alisema Mtendaji huyo.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo akiwamo Mary Peter, alisimulia kuwa baada ya vurugu hizo yeye na watoto wake walijificha uvunguni mwa kitanda kujinusuru.

**TUME YALAANI**

Kutokana na tukio hilo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imelaani kitendo cha wananchi kujichukulia sheria mkononi.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, amewataka wananchi kuwa wavumilivu na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria katika kukabiliana na masuala ya namna hiyo.

# Biteko atangaza neema kushuka bei gesi ya kupikia

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema serikali inafanya kila linalowezekana kushusha bei ya gesi ya kupikia, ili ipatikane kwa gharama nafuu kwenye maeneo yote nchini.

Amesisitiza kuwa wananchi wanataka huduma bora, vyeo na mamlaka walizonazo havina maana kama watanzania watapata huduma hafifu.

Dk. Biteko aliyasema hayo jana jijini hapa katika hafla ya uzinduzi wa jengo la Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na utiaji saini mikataba sita ya utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa matumizi ya nishati safi za kupikia.

Miongoni mwa mikataba hiyo ni wa kusambaza mitungi 450,000 ya gesi ya kilo sita katika maeneo ya vijiji na pembezoni mwa miji utakaotekelezwa na kampuni za Manjis, Oryx, Lake Gas na Taifa Gas ambapo serikali kupitia REA, itatoa ruzuku ya hadi asilimia 50 kwa wananchi ili kununua mitungi hiyo.

Naibu Waziri Mkuu alisema Rais Samia Suluhu Hassan amewapa maelekezo mahsusi, kwamba waangalie kila aina ya fursa iliyoko ya kufanya nishati safi ya kupikia ipatikane kila mahali na watanzania waipate.

"Kuna wakati mtu anaonesha ugumu, anasema ajenda hamuiwezi kwa sababu bei ni kubwa, ni kweli ni kubwa lakini serikali inafanya kila linalowezekana kuishusha ili nishati hii ipatikane kwa unafuu katika maeneo yote.

"Tumeanza na hii mitungi zaidi ya 400,000 itakayopatikana kwa bei ndogo na ziko nishati nyingine ambazo zinapatikana kwa bei nafuu," alisema.

Kuhusu mikataba iliyotiwa saini, Dk. Biteko alitaka ikawe kichocheo kwa kuhakikisha kwamba, malengo ya serikali ya kufikia asilimia 80 ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

"Itakuwa aibu sana leo kutia saini hapa halafu baada ya muda watanzania wasione matokeo, watanzania wanatarajia kuona matokeo ya haraka nishati safi ya kupikia ni ajenda ya kuokoa maisha ya watu,"alisema.

Kadhalika, alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, kuhakikisha majengo yote ya wizara yanatumia nishati ya umeme jua na kuwa mfano kwa taasisi zingine za serikali, ili kupunguza gharama za uendeshaji.

"Sisi wizara ambao tunawaambia watu kila wakati tutumie nishati safi, hivi ni kwa kiasi gani sisi katika ofisi zetu tunatumia nishati safi, ninataka nione majengo yote ya wizara tuwe mfano wa kutengeneza 'provision ya solar' ili mchana tutumie solar, usiku tena mara nyingine hata usiku hatupo matumizi yawe kidogo tuwe mfano kwa taasisi nyingine za serikali tuanza sisi," alisema.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, alisema magereza yameanza kutekeleza matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuondokana na matumizi ya kuni kama chanzo kikuu kwa asilimia 98.

Alisema jeshi hilo lilianza kuhama katika matumizi hayo kuni na mkaa baada ya kubaini madhara na ilianzisha mradi wa matumizi majiko banifu ambayo yalipunguza matumizi ya kuni kwa asilimia 40 kati ya mwaka 2016 hadi 2019.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Hassan Saidy, alisema mikataba hiyo sita yenye thamani ya Sh. bilioni 72.8, pia inahusisha kujenga na kusambaza mifumo ya nishati safi katika Jeshi la Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Kuhusu jengo la REA, alisema limejengwa kwa miezi 18 kwa gharama ya Sh. bilioni 9.8 badala ya Sh. bilioni 13 iliyopangwa awali na hivyo kuokoa kiasi cha Sh. bilioni 3.2.



Wafanyabiashara wadogo wakiwa wamepanga vibanda vyao hadi kwenye eneo la barabara na kuifanya kuwa finyu nyuma ya kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam na kusababisha usumbufu mkubwa kwa magari, pikipiki, baiskeli na waenda kwa miguu, kama ilivyonaswa na kamera yetu, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwalimu kortini madai ya kulawiti mwanafunzi

**Na Halima Ikunji,**
TABORA

MWALIMU Denin David (23), mkazi wa Kata ya Bomba Mzinga, Manispaa ya Tabora, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Tabora akikabiliwa na shtaka la kumlawiti mwanafunzi aliyekuwa akimfundisha masomo ya ziada (twisheni).

Akisoma shtaka hilo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi John Mdoe, Wakili wa Jamhuri, Charles Magonza, akisaidiwa na Wakili Steven Mnzava, alidai mshtakiwa alimlawiti mwanafunzi wake wa kiume wa darasa la tano (jina la mwanafunzi na shule vinahifadhiwa) wakati akimfundisha masomo ya ziada nyumbani kwake.

Alidai mshtakiwa huyo alikuwa akimfundisha wanafunzi huyo na wenzake masomo ya ziada ya Hesabu na Sayansi na kumlazimisha kumwingilia kinyume na maumbile.

Aidha, alidai kuwa kosa hilo ni kinyume cha Sheria Namba 154 ya Makosa ya Adhabu Sura 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Kupitia kifungu hicho cha sheria ambacho kinasema wazi mtu yeyote atakaye mwingilia mtu kwa lazima ama kwa hiyari yake, adhabu yake ni kifungo cha maisha jela.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, alilikana kosa hilo ambalo dhamana yake iliwekwa wazi kutokana na kukidhi vigezo na kosa hilo kudhaminika.

Hakimu Mkazi Mwandamizi Mdoe aliahirisha shauri hilo mpaka litakapoitwa Septemba 28, mwaka huu huku mshitakiwa huyo akipata dhamana.

# Wahudumu waraibu kupimwa dawa za kulevya

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) inatarajia kuanza kuwapima wanaohudumia vituo vya waraibu wa dawa hizo.

Hali hiyo unatokana na baadhi ya watumihi wa waraibu wanaokaa katika makazi hayo kukutwa na viashiria vya dawa za kulevya.

Aidha, imesisitiza kujenga kwa vituo hivyo katika maeneo ya Kahama kutokana na kuwa na waraibu wengi.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Aretas Lyimo, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wamiliki wa vituo hivyo nchini katika mkutano uliofanyika jijini hapa.

Lyimo alisema lengo la kufanya hivyo ni kutokomeza matumizi ya dawa hizo ili wale wanaotumia wapone na kuhakikisha wahudumu hawaingizi dawa katika vituo wanavyohudumia.

“Tunatarajia kuanza kuwapima wanaohudumia sober house (vituo vya waraibu) kwa sababu wanaokaa katika vituo hivyo wakipimwa, baadhi yao wanakutwa na viashiria vya dawa za kulevya ilihali wapo ndani ya nyumba hizi.

“Kila mmoja anapaswa kuwa mlinzi wa mwenzie, tukifanya hivyo tutaweza kutokomeza matumizi ya dawa za kulevya nchini,”alisema.

Pia, aliwataka wahudumu kuacha kuwapiga waathirika wa dawa hizo na badala yake wawape tiba inayostahili ili wapone.

“Ninaomba watu wafungue Sober House katika maeneo ambayo hayana, kwa mfano eneo la Kahama mkoani Shinyanga, kuna waraibu wengi kutokana na kwamba, mji ule ni wa kibiashara hivyo unakutanisha watu kutoka mataifa tofauti.

“Pale kuna waraibu wengi sana na wanaathirika kiasi kikubwa, hivyo pale panahitaji uwapo wa sober house ili kuwasaidia waraibu wa dawa za kulevya,”alisema.

Alibainisha kuwa hivi sasa kuna vituo 62 na waraibu 17,000 wamesaidiwa.

Naye Kamishna Msaidizi wa Dawa za Kulevya Kanda ya Kati, Mzee Kasuwi, alihimiza wamiliki na watoa huduma katika vituo hivyo kufuata masharti ya kuhudumia waraibu na serikali itaendelea kuwa pamoja nao.




Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Juma Kijavala (kushoto), akitoa maelekezo kwa Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa alipotembelea mradi wa ujenzi wa matangi maalum ya kuhifadhia mafuta katika Kata ya Tungi, wilayani Kigamboni, Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbarawa atembelea eneo ujenzi matangi kuhifadhia mafuta TPA

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, ametembelea mradi wa ujenzi wa matangi maalum ya kuhifadhia mafuta (Oil Terminal) wa Mamlaka ya Usimamzi wa Bandari Tanzania (TPA) unaofanyika katika Kigamboni, Dar es Salaam.

Ujenzi huo unahusisha matangi makubwa 15 yenye uwezo wa kuhifadhi ujazo wa lita 378,000 za mafuta pindi yanapoingizwa nchini na kuumwagia sifa utekelezaji wake.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo katika eneo la ujenzi lililoko katika kata ya Tundwi, Prof. Mbarawa alisema ujenzi huo utakaochukua muda wa miaka miwili, utasaidia katika kuboresha ufanisi wa bandari.

Prof. Mbarawa alisema utasaidia kupunguza foleni ya meli za kupakua mafuta. Meli moja hutozwa wastani wa faini ya Sh. milioni 50 kwa siku wakati ikiwa katika foleni ya kupakua mafuta hayo.

Kwa mujibu wa Prof. Mbalawa, ufinyu wa matangi ya kuhifadhia mafuta ulisababisha wasafirishaji kutozwa kiasi kikubwa cha pesa na mwisho wa siku gharama hizo pia ziliwagusa wananchi.

“Wakati mwingine meli hulazimika kusubiri kupakua mafuta hata zaidi ya wiki moja, hii inaonyesha ni kwa kiasi gani wasafarishaji wa mafuta wanaumia na faini hii,” alisema.

Prof. Mbalawa alisema ili kuifanya bandari ya Dar es Salaam kuwa moja ya bandari zenye ushindani duniani, serikali imeamua kufanya ujenzi huo wa matangi 15 ambao sasa meli hizo zitatumia saa chache kupakua nishati hiyo na kuondoka.

Alisema ujenzi huo utafanya kazi ya usambazaji wa mafuta hayo kwenda kwa wateja (kampuni za kuuza mafuta) kwa urahisi sana na kukabiliana na uhaba wa mafuta unaoweza kutokea.

Pia, alisema ujenzi wa matenki hayo utaifanya Serikali kuwa na hifadhi ya kutosha ya nishati hiyo kwa ajili ya usalama wa nchi.

“Nikiwa kama Waziri wa Uchukuzi, nimefurahi sana kuona mradi huu hatimaye unatekelezwa na ninaupongeza sana uongozi wa TPA kwa hatua hii.

“Tulijaribu mara kadhaa huko nyuma lakini tulishindwa, ila mipango thabiti ya bodi na uongozi wa TPA umesababisha kutekelezwa kwa mradi huu,” alisema Prof. Mbarawa.

Meneja wa mradi huo, Mhandisi Hamis Mbutu, alsema mradi huo unatarajiwa kumalizika kwa wakati na kuwa na tija kwa bandari hiyo na Serikali kwa ujumla katika kukusanya ushuru.

Awali, Mkurugenzi Msaidizi wa TPA, Juma Kijavara, alisema mkataba wa ujenzi huo wenye thamani ya shilingi bilioni 678.6 ulisainiwa rasmi Februari 26, 2024. Tayari mkandarasi China Railway Major Bridge Engineering Group ameshalipwa Sh. bilioni 9.9 kuanza ujenzi huo.

Akimwelezea Prof. Mbarawa hatua za utekelezaji wa mradi huo, Mhandisi Wen Hongyuan kutoka China Railway alisema kwa sasa upo asilimia tano ya utekelezaji na tayari kazi ya kusafisha eneo la ujenzi na ofisi za wajenzi zimekamilika.

Alisema ujenzi huo utahusisha matangi sita kwa ajili kuhifadhia mafuta aina ya dizeli, Matano kwa ajili ya petroli na matatu ya kuhifadhia mafuta ya kuendeshea ndege.

# ‘Mchakato wa kuhama kwa hiari Ngorongoro bado uko pale pale

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, amesema kuwa mchakato wa kuhama kwa hiari kwa wananchi wa Ngorongoro unaendelea huku akisisitiza kwamba, serikali inafanya maboresho mbalimbali ili kurahisisha suala hilo.

Balozi Chana aliyasema hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro katika Makao Makuu ya Ofisi za NCAA Wilayani Karatu Mkoani Arusha.

“Niseme tu kwamba mchakato wa kuhama kwa hiari unaendelea na maboresho yanaendelea na kuna maeneo ya Kitwai, Kilindi na sehemu nyingine ambazo watu wanapenda kwenda wanakwenda kwa hiari,” alisema.

Aliwataka askari uhifadhi kusimamia vyema mchakato huo ili kurahisisha utekelezaji wake.

Aidha, aliwataka kuendelea kufuata maelekezo mbalimbali ya serikali ikiwa ni pamoja na kuboresha utoaji wa huduma za kijamii kwa wananchi kama geti na vyoo vya wanafunzi.

Katibu Mkuu wizara hiyo, Dk. Hassan Abbasi, alisema hifadhi hiyo imeongeza idadi ya watalii kwa asilimia 21 kwa takwimu za mwezi Januari hadi Juni, 2024, watalii wa nje walikuwa 180,000 mpaka 200,000 huku akisisitiza kuwa Wizara imeendelea kutimiza wajibu wake katika kuisimamia NCAA.

Alisema kuwa pamoja na mafanikio hayo, Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya azimio kubwa la kutoa asilimia tatu ya mapato kwa ajili ya uhifadhi na asilimia sita kwa ajili ya kutangaza utalii.

Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Dk. Elirehema Doriye, aliipongeza wizara hiyo kwa kuendelea kusimamia vizuri kazi mbalimbali za mamlaka hiyo.

**Aliwataka askari uhifadhi kusimamia vyema mchakato huo ili kurahisisha utekelezaji wake.**

# Bilioni 3.9/- kuimarisha miundombinu ya hifadhi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 3.9 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu katika Hifadhi ya Taifa Ibanda - Kyerwa iliyoko mkoani Kagera.

Akikagua miradi ya ujenzi wa miundombinu hiyo, Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Musa Kuji, alisema serikali ilitoa fedha hizo kwa ajili ya kujenga lango la kuingilia watalii na nyumba za kisasa za watumishi eneo la Kifursa.

"Hili ni deni kwetu TANAPA hususani watumishi wa hifadhi hii na tutamlipa kwa kuchapa kazi na kujituma zaidi katika kulinda na kutunza rasilimali hizi kwa faida ya kizazi cha sasa na kile cha baadaye," alisema Kamishna Kuji.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Fredrick Mofulu, ambaye ni Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ibanda - Kyerwa, alisema ujenzi wa lango hilo la hifadhi unahusisha sehemu ya ukaguzi wa nyaraka na malipo, ofisi za wahasibu, ofisi za askari upande wa kuingia na kutokea, ofisi ya ofisa utalii na msaidizi wake, ofisi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ujenzi wa barabara kilometa mbili, na mifumo ya umeme.

Pia inahusisha ujenzi wa vyoo upande wa kuingia, na kutokea vyenye mashimo saba ya kawaida moja walemavu kwa kila jengo, uchimbaji wa visima viwili, fensi ya umeme mita 400, nyumba mbili za watumishi (jengo moja kwa familia mbili).

Nyingine ni nyumba tatu za watumishi (jengo moja kwa familia nne), vimbweta nane, sehemu ya kupaki magari makubwa na madogo upande wa kutoka na kuingia lenye ukubwa wa kilometa za mraba 5400, mfumo wa umeme jua, pamoja na eneo la kupumzikia wageni.

Alisema kazi hiyo ilifanywa na Kampuni ya MJT Crew Co. na JV Sumry's Enterprises Ltd za nchini na mpaka sasa ujenzi uko asilimia 55 na inatarajiwa kukamilika Novemba, mwaka huu.

Msimamizi wa Mradi kutoka kampuni ya MJT Crew, Mhandisi Issa Mfaume, aliishukuru menejimenti ya TANAPA kwa kuwapatia malipo ya mradi kwa wakati na kupelekea kazi kufanyika kwa ubora unaotakiwa na kuahidi kukamilisha kazi hiyo kwa wakati na kwa kuzingatia viwango vilivyopo kwenye mkataba wa kazi.

Kamishna Kuji alizungumza na maafisa na askari wa Jeshi la Uhifadhi wa Hifadhi ya Taifa Ibanda - Kyerwa na Hifadhi ya Rumanyika - Karagwe na kusitiza utendaji kazi imara ili kusukuma mbele gurudumu la uhifadhi na utalii ambalo tumekabidhiwa na serikali.

"Wapiganaji ndio nguzo ya kupeleka mbele Shirika letu nitoe pongezi zangu za dhati kwa askari wetu ambao jua ni lao na mvua ni yao kuhakikisha rasilimali hizi zinalindwa na kuwa urithi kwa vizazi vilivyopo na vijavyo," alisema Kamishna Kuji

Aidha, Kamishna Kuji alisisitiza kuwa kila mtumishi ana haki ya kujiendeleza kielimu, haki ya kulipwa posho kwa kila kazi aliyoifanya, haki ya matibabu, likizo, haki ya kupandishwa cheo pale unapotimiza vigezo vyote vya kiutumishi pamoja na haki ya kuthaminiwa kutokana na kazi unayofanya.

Wapiganaji kwa namna mbalimbali wamepongeza jitihada zinazofanywa na taasisi katika kutatua changamoto zao na kupongeza namna viongozi wanawafikia katika maeneo yao, wanasikiliza na kutatua changamoto hizo.

"Nikupongeze Afande Kamishna Kuji licha ya majukumu uliyonayo unatoka na kuja kuzungumza na askari, tumekuona Serengeti, tumekuona Saanane, sasa Ibanda Kyerwa na Rumanyika Karagwe. Ukaribu huu kwetu kama askari na kiongozi wa juu wa taasisi unatia hamasa na morali zaidi ya kuchapa kazi" alisema askari wa uhifadhi daraja la kwanza Henry Msabila.

## Pinda akabidhi wajasiriamali hundi mil. 45/-

**Na Munir Shemweta,** MLELE

MBUNGE wa Kavuu na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amekabidhi hundi ya Sh. milioni 45 kwa vikundi vitatu vya wajasiriamali wa halmashauri ya Mpimbwe, Mlele mkoani Katavi kutoka benki ya CRDB ili kuvijengea uwezo.

Pinda alikabidhi hundi hiyo juzi wakati akifungua semina ya siku moja ya kuvijengea uwezo vikundi vya wajasiriamali vya wanawake na vijana kunufaika na programu ya IMBEJU katika kata za halmashauri ya Mpimbwe iliyofanyika kata ya Majimoto.

Vikundi vilivyokabidhiwa kiasi hicho cha fedha ni Nguvumoja Kashishi, Imani Kashishi na kikundi kingine kitakachokidhi vigezo vya kuwezeshwa.

Akizungumza wakati wa kuzindua semina hiyo, Pinda amesema ili kuendesha biashara kisasa ni lazima wajasiriamali wapate ushauri na mafunzo kutoka kwa wataalamu.

Alisema taasisi za fedha kama CRDB ni miongoni mwa sehemu ya uhakika ambayo mjasiriamali anaweza kupata elimu ya fedha ya uhakika ili kufanikisha mipango ya biashara.

Pinda aliwataka wajasiriamali wa Mpimbwe kutumia fursa inayolingana na uwezo wao binafsi na si kusikia tu benki inatoa mitaji wezeshi na kulazimika hata kudanganya ili kukopa fedha pasipo mikakati makini ya kuzitumia.

Aliishukuru CRDB kupitia taasisi yake ya CRDB Foundation kwa ubunifu wa kuwafikia wajasiriamali wadogo hata waliopo pembezoni kama vile Mpimbwe.

"Hili si jambo dogo kwa taasisi inayojiendesha kibiashara kutenga bajeti ya kuelimisha wananchi na kuwapa mitaji wezeshi" alisema.

Washiriki wa semina hiyo ya siku moja wametoka kata za Kasansa, Mamba, Majimoto, Mwamapuli, Chamalendi, Mbede, Ikuba, Usevya pamoja na Kibaoni katika halmashauri ya Mpimbwe wilaya ya Mlele mkoa wa Katavi.

## Zamu ya Dodoma, Manyara, Singida daftari la kudumu la wapigakura

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imetangaza kuanza uboreshaji wa Daftari la Kudumu la WapigaKura kwa mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara huku ikiwataka wananchi kuepuka kujiandikisha zaidi ya mara moja kwa kuwa ni kosa kisheria.

Mjumbe wa INEC na Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Omari, alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa tume hiyo na wadau wa uchaguzi mkoa wa Singida kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura .

Alisema mzunguko wa tano wa uboreshaji ambao utajumuisha mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara utaanza Septemba 25 hadi Oktoba Mosi, mwaka huu. Vituo vya kutekeleza kazi hiyo vitakuwa vinafunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi 12:00 jioni.

"Kujiandikisha kuwa mpigakura zaidi ya mara moja ni kosa la kisheria kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 114(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais,Wabunge na Madiwani namba moja ya 2024," alisema.

Jaji Omari alisema kifungu hicho cha sheria kinaeleza kuwa mtu yeyote atakayeomba kuandikishwa zaidi ya mara moja atakuwa ametenda kosa la kisheria na akitiwa hatiani adhabu yake ni faini isiyopungua Sh.100,000 na Sh.300,000, kifungo kisichozidi miezi mitatu, miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Alisema ili kufanikisha uboreshaji huo, wadau wa uchaguzi ni muhimu kutoa ushirikiano kwa tume na kuwa mabalozi wazuri wa kusambaza taarifa na kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na kuboresha taarifa zao ili zoezi lifanyike kwa ufanisi na kwa mafanikio makubwa.

Aliongeza kuwa mawakala au viongozi wa vyama vya siasa hawaruhusiwi kuingilia mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura vituoni.

"Niwaombe viongozi wa vyama vya siasa na wadau wa uchaguzi kwa ujumla kuzingatia sheria za uchaguzi, kanuni za uboreshaji,maelekezo ya tume na kusimamia miiko na mipaka ya uendeshaji wa zoezi la uboreshaji wa daftari," alisema.

Jaji Omari alisema viongozi wa vyama vya siasa kama kutakuwa na changamoto zitakazojitokeza watumie sheria zilizopo kuwasilisha kwa tume ambapo Tume ya Taifa ya Uchaguzi itazingatia katiba,sheria ya uchaguzi na kanuni zilizotungwa chini ya sheria katika zoezi la uboreshaji.

Naye Mkurugenzi wa Uchaguzi, Kailima Ramadhani, alisema uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa mikoa yote unatarajiwa kukamilika Machi, 2025.

Alisema kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, wapigakura 5,586,433 wapya wanatarajiwa kuandikishwa sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,699 walioko kwenye daftari baada ya uboreshaji uliofanyika mwaka 2019/20.

Kailima alisema wapigakura 4,369,531 inatarajiwa wataboresha taarifa zao, wapigakura 594,494 inatarajiwa wataondolewa kwenye daftari kwa kukosa sifa za kuendelea kuwapo kwenye daftari, hivyo baada ya uboreshaji, inatarajiwa daftari litakuwa na wapigakura 34,746,638.

Alisema katika kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa, tume imeshakamilisha maandalizi ya idadi ya vituo 40,126 vya kuandikisha wapiga kura ambavyo vitatumika katika uboreshaji wa daftari 2024.

"Vituo 39,709 viko Tanzania Bara na 417 viko Zanzibar. Hili ni ongezeko la vituo 2,312 ikilinganishwa na vituo 37,814 vilivyotumika 2019/20," alisema.




Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kulia), akikaribishwa na kukabidhiwa zawadi na Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa Kampuni ya Tigo, Mwangaza Matotola wakati alipofanya ziara ya kikazi katika kampuni hiyo, Dar es Salaam juzi. **PICHA: FAUSTINE FELICIAN**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusimalize maneno kwa Stars, tuendelee kuiunga mkono

**TIMU** ya taifa 'Taifa Stars' bado ipo kwenye kampeni ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Afrika (AFCON) za mwaka 2025 zitakazofanyika nchini Morocco.

Tunasema Taifa Stars bado wapo kwenye kampeni za kusaka tiketi hiyo kwa sababu ya matokeo waliyoyapata kwenye mchezo wa hivi karibuni dhidi ya Guinea.

Stars ikiwa ugenini, Ivory Coast Jumanne iliyopita ilifanikiwa kupata ushindi muhimu na wa kusisimua wa mabao 2-1 dhidi ya Guinea ambao walichagua mchezo huo kuuchezea huko kutokana na viwanja vya kwao kutokidhi vigezo vya Shirikisho la soka Afrika, CAF.

Kabla ya mchezo huo, Stars ilikuwa imetoka suluhu na Ethiopia kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, matokeo hayo yaliibua maneno maneno mengi kutoka kwa mashabiki na wadau mbalimbali wa soka.

Matokeo hayo na mchezo uliotajwa kuwa wa kutovutia dhidi ya Waethiopia hao yaliwagawa mashabiki ambapo wapo walioona Stars wana wakati mgumu na pengine hawana matumaini ya kupata tiketi ya kushiriki AFCON ya Morocco.

Lakini pia wapo waliokuwa na matumaini huenda michezo inayofuata Stars ikafanya vizuri na kuendelea kuweka hai matumaini ya kufuzu fainali hizo.

Kimsingi maneno yalikuwa mengi na wapo pia walioanza kulishambulia benchi la ufundi na kusema hawana imani nao katika safari ya kuwapeleka Morocco.

Jambo tunalotaka kusema ni kwamba, hatupaswi kumaliza maneno pale timu yetu inapopata matokeo yasiyotufurahisha , tunapaswa kuendelea kusapoti timu yetu katika kila hali.

Matokeo ya Jumanne iliyopita mbele ya Guinea yametupa majibu hayo, wale waliokuwa wakiibeza na kuikatia tamaa walikosa cha kuongea, lakini wale waliokuwa na matumaini na kuendelea kuiunga mkono ndio waliokuwa na furaha ya kweli.

Timu ya taifa ni timu yetu sote watanzania, sio timu ya mashabiki wa Simba, Yanga wala Pamba, ni timu ya kila Mtanzania bila kujali dini wala kabila lake, tunapaswa kuiunga mkono sote.

Taifa Stars ikipata ushindi ni ushindi wa Watanzania, na hata ikipoteza mchezo ni Tanzania ndio iliyopoteza, tuwe na akiba ya maneno kwa timu yetu.

Nipashe tunawakumbusha mashabiki, kuelekea kukamatia tiketi ya kushiriki AFCON ya 2025, Stars bado ina kazi kubwa mbele yake kwa kuwa kuna michezo mingine minne mbele yake katika Kundi H walikopangwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Ethiopia na Guinea.


Mchezo unaofuata Stars itacheza na vinara wa kundi lao, Congo, ni lazima sasa watanzania tuungane na kuiunga mkono timu yetu kwa kuwatia moyo wachezaji pamoja na kujitokeza kwa wingi uwanjani kila inapocheza kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

Katika michezo minne iliyobaki, Stars ina michezo miwili watakayocheza nyumbani, tujipange kujitokeza kwa wingi kuhakikisha tunakata tiketi ya kushiriki fainali hizo.

Ikumbukwe, baada ya fainali za Morocco, Tanzania kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda tutakuwa wenyeji wa fainali za mwaka 2027, hivyo kushiriki kwetu fainali za 2025 kuna maana kubwa sana.

Hongereni wachezaji Taifa Stars kwa ushindi dhidi ya Guinea, lakini pia mkumbuke watanzania tupo nyuma yenu na tunatarajia makubwa zaidi katika kampeni ya kufuzu fainali hizo za Morocco.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Aibu, Taifa Stars wametusuta

**WAZARAMO** wana msemo wao, 'usinene ukamala', ukiwa na maana usiongee ukamaliza maneno kwani yanaweza kukurudia. Msemo huu una maana nyingi, ikiwemo kwamba unaweza kumsema na kumlaumu mtu, lakini kumbe ikawa sivyo ulivyodhani, au ikawa ni bahati mbaya tu. Mara nyingi ikija kudhihirika kwamba si kweli kwa jinsi ulivyomtuhumu unabaki na aibu.

Hili limeonekana Jumanne iliyopita, baada ya Taifa Stars kuwaumbua wahafidhina wote waliokuwa wameongea maneno mengi kuhusu timu hiyo.

Kuanzia mashabiki wa soka, mpaka baadhi ya wachambuzi walikuwa wameikatia tamaa Stars baada ya suluhu nyumbani dhidi ya Ethiopia, Septemba 4, ambapo kila mmoja hakutarajia kama ingeweza kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Guinea.

Suluhu dhidi ya Ethiopia ilizua mengi sana. Wengine waliponda kikosi kilichopangwa na makocha Hemed Suleiman 'Morocco' na msaidizi wake, Juma Mgunda. Wapo waliosema Stars haishindi kwa sababu wachezaji wengi wa kikosi hicho hawapati namba kwenye timu zao za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wapo waliohoji hata kwa nini Stars ina makipa Ali Salim wa Simba na Abutwalib Mshery wa Yanga ambao kwenye vikosi vya timu zao siyo makipa namba moja.

**Wapo waliohoji hata kwa nini Stars ina makipa Ali Salim wa Simba na Abutwalib Mshery wa Yanga ambao kwenye vikosi vya timu zao siyo makipa namba moja.**

Ushauri wao ukawa iletwe kanuni ya kuwaondoa makipa wote wa kigeni kwenye ligi na wadake wazawa tu. Yote hii ilikuwa ni hasira ya Stars kutopata ushindi.

Sasa wapo waliodhani kuwepo kwa wachezaji 12 wa kigeni kunawawafanya wazawa wakose nafasi kwenye vikosi vyao na hii inasabisha Stars isiwe na kikosi cha wachezaji bora, hivyo wapunguzwe au waondolewe kabisa.

Bado wapo mashabiki wanaodhani kuwa Tanzania haina uchaguzi sahihi ya wachezaji bora, ndiyo maana inaonekaa kama haina wachezaji wenye viwango.

Mambo yalikuwa mengi sana, wengine walianza kuorodhesha hata wachezaji wa Kitanzania waliopo nje ya nchi nao waitwe ili waokoe jahazi la Stars, wengine wakaishauri Serikali kukubali uraia pacha ili Tanzania iwe na wachezaji wenye uraia wa nchi mbili kwani wapo wachezaji wa aina hiyo na ni wengi huko nje ya nchi.

Presha ilikuwa kubwa sana. Kuanzia kwa mashabiki, wachambuzi, makocha na wachezaji wa Stars ikawa ni presha kila mahala.

Ikaonekana kama haitokuwa na uwezo wa kufanya vyema, na hata mechi dhidi ya Guinea wengi waliikatia tamaa.

Baada ya kushinda kila mmoja sasa anameza maneno yake. Wote waliopoonda sasa wanasifu. Unaweza kudhani kama siyo wale waliokuwa wanaponda.

Hatusikii tena wachezaji wa kigeni wanazuia wazawa kwenye ligi, wala kupunguzwa na makipa kutoka nje ya nchi.

Hii inatufundisha mashabiki wa soka kuwa na subira kwa sababu soka ni mchezo wenye matokeo matatu, kushinda, sare na kupoteza. Na mpira unaweza kushinda popote pale.

Inatufundisha pia mashabiki wa soka na wachambuzi kufanya tathimini za kimpira na za kisayansi na si za kimihemko.

Kushinda Taifa Stars, kufungwa au sare, hakuhusinai na wingi au uchache wa wachezaji wa kigeni, badala yake ni matokeo tu ya mpira.

Haya Stars imeshinda, wachezaji 12 wa kigeni na kipa wao wameondoka? Ifike wakati mashabiki wa soka na wachambuzi wasiongee na kumaliza maneno ya sababu ya mihemko. Juzi tumeiponda Stars, leo imeshinda maneno yameturudia wenyewe, tunayakana, tunaisifia Stars.

## STANBIC yajivunia kushiriki wiki AZAKi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imesema inajivunia kushiriki katika Wiki ya Asasi za Kiraia (Azaki) ya mwaka huu, tukio lenye ushawishi mkubwa linalowaleta pamoja mashirika ya kiraia (Azaki), wadau wa serikali, na viongozi wa sekta binafsi kushirikiana na kuendeleza ajenda ya maendeleo endelevu ya Tanzania.

Tukio hilo lilianza Septemba 9, mwaka huu na kumalizika jana Arusha likiwa na kaulimbiu ya "Sauti, Dira, Thamani", wito wa kuchukua hatua ambao unalingana kikamilifu na dhamira ya benki ya Stanbic ya kuwezesha jamii, kukuza ujumuishaji wa kifedha, na kuunga mkono malengo ya Dira ya Tanzania 2050.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Doreen Dominic, Mkuu wa Sekta ya Umma katika Benki ya Stanbic, alisisitiza umuhimu wa ufadhili endelevu katika kuchochea ukuaji wa Tanzania.

"Wiki hii ni kumbukumbu yenye nguvu wa mshikamano kati ya Azaki na jukumu muhimu walilonalo katika kuendeleza malengo ya maendeleo ya Tanzania," alisema Dominic. "Kaulimbiu ya 'Sauti, Dira, Thamani' inafafanua vizuri dhamira yetu ya pamoja ya kuunda mustakabali jumuishi na wenye ustawi.

"Kwa Benki ya Stanbic, hatujishughulishi tu na masuala ya kifedha bali tumewekeza katika ukuaji wa muda mrefu wa kutoa suluhisho maalum la kifedha litakalowezesha jamii nchini,"alisema.

Ushiriki wa benki ya Stanbic katika Wiki ya Azaki unaonyesha kujitolea kwake kwa dhati katika kuchochea uchumi jumuishi kwa kupitia programu kama Biashara Incubator na Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Wanawake, benki imekuwa mstari wa mbele katika kusaidia wakulima wadogo na wajasiriamali, na kuchangia ongezeko la 40% katika uthabiti wa kiuchumi wa walengwa.

Dominic alisisitiza kuwa programu hizi zinaonyesha dhamira ya Stanbic kuhakikisha kuwa Watanzania wote wanapata nyanja za kifedha wanazohitaji ili kufanikiwa.

"Jukumu letu wiki hii ni kuendelea kuwawezesha Watanzania kupitia suluhisho maalum zinazochochea athari chanya za muda mrefu," alisema. Pia alisisitiza kuwa jukumu muhimu katika mijadala juu ya haki ya kiuchumi ya wanawake, hasa kupitia msaada wake kwa bajeti zinazozingatia jinsia.

Dominic alisisitiza kuwa kufikia usawa wa kijinsia ni jambo muhimu kwa maendeleo endelevu ya Tanzania.

"Kuwawezesha wanawake ni ufunguo wa kujenga jamii yenye haki na ustawi zaidi," Dominic aliendelea kusema katika hotuba yake.

"Kwa kushughulikia changamoto za kipekee wanazokabiliana nazo wanawake na kuhakikisha ugawaji wa rasilimali kwa haki, tunaweza kuunda mazingira ambamo kila mtu, bila kujali jinsia, anapata fursa ya kufanikiwa," alisema.

Moja ya vivutio muhimu vya ushiriki wa Benki ya Stanbic katika Wiki ya Azaki ni mtazamo wao juu ya Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika (AfCFTA).

Dominic alielezea kwamba biashara za kikanda na ukuzaji wa rasilimali watu ni muhimu kwa kuhakikisha mustakabali wa kiuchumi wa Tanzania. "Benki ya Stanbic imejitolea kusaidia biashara za Kitanzania, hasa zile ndogo na za kati (SMEs), katika kunufaika na fursa zinazotolewa na AfCFTA. Kwa kuboresha utayari wa biashara za kuvuka mipaka na kuendeleza ujuzi muhimu, tunasaidia kuiweka Tanzania kama muhusika muhimu katika soko pana la Afrika," alibainisha.

Wiki ya Azaki inaendelea, Benki ya Stanbic itaendelea kushiriki katika mijadala muhimu kuhusu ukuaji endelevu, maendeleo jumuishi, na ushirikiano wa muda mrefu na Azaki.




Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi na Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano na Wadau wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Victor Byemelwa (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro juzi, kuhusu maonesho ya Siku ya Wakulima wa Miwa wa Bonde la Kilombero, yanayotarajiwa kuanza Oktoba 10 hadi 12 mwaka huu. Kushoto ni Meneja wa Kilombero Joint Enterprises Cooperatives Society, James Mayunga na Meneja kutoka Shirika la African Wildlife Foundation, Clarence Msafiri. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mashahidi 40, vielelezo 480 kuwasilishwa kesi kuisababishia hasara TRA MIL. 971.7/-

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kinondoni, inatarajia kusikiliza mashahidi 40 na kupokea vielelezo 480 katika kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili wakazi wanne wa Dar es Salaam, wanaodaiwa kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. milioni 971.7

Washtakiwa hao ni Frank Kagale, fundi wa mashine za kielektroniki (EFD), Awadhi Mhavile (39), Ally Msesya maarufu kama Ally Yanga (37) Mkazi wa Pugu na Salma Ndauka (38), mkazi wa Sinza na Msimamizi wa Gereji wanakabiliwa Na mashtaka 574 yakiwamo ya kughushi.

Wakili wa Serikali, Tumpale Lawrence, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Emmanuel Medalakini, na Wakili wa Serikali Auni Chilamula, alidai mbele ya Hakimu Is-haq Kuppa kuwa shauri hilo juzi lilikuja kwa ajili ya kusikilizwa hoja za awali kufuatia upelelezi kukamilika.

Akisoma hoja hizo, Wakili Tumpale alidai mbele ya Hakimu Mfawidhi Kuppa kuwa Machi, 2023 TRA ilipokea taarifa kutoka kwa msiri kuwa kuna risiti za kielektroniki zilizotolewa kutoka kwenye mashine zilizopotea au kuibwa kutoka kwa wamiliki halali na zinasambazwa isivyo halali.

Anadai kuwa, kutokana na taarifa hiyo uchunguzi ulianza kwa kushirikiana na maofisa wa Jeshi la Polisi na ndipo Julai 7, 2023 mtu aitwaye Meshack Athanas, dereva wa pikipiki maarufu kama bodaboda alikutwa na risiti za kielektroniki saba za Sh 128,500,000.

Pia, alidai kati ya risiti hizo nne zilikuwa zimetolewa kutoka kwenye mashine ya kieletroniki mali ya Africa Harmony and Trade Ltd yenye namba 03TZ843040152 aliyesajiliwa kwa namba ya mlipakodi 159265420.

"Risiti mbili zilitolewa kutoka kwenye mashine ya kieletroniki mali ya Tabisco Entreprises ltd yenye namba 03TZ442007272 na namba ya mlipa kodi ni 100219557 na risiti moja iliyotolewa kutoka kwenye mashine ya kieletroniki mali ya Eco Consumer Products ltd yenye namba 03TZ442021550. Katika maelezo ya Athanas alieleza kupewa risiti hizo na Ally Omary Msesya ambae ni mtuhumiwa namba tatu," alidai Tumpale.

Katika tarehe hiyohiyo, ilidaiwa kuwa Athanas aliwaongoza wapelelezi katika ukamataji wa mshtakiwa Msesya na Julai 8, 2023 Athanas aliwaongoza wapelelezi kumkamata mshitakiwa Mhavile.

Alidai kuwa, baada ya kukamatwa mshtakiwa Mhavile alikutwa na risiti za kieletroniki 11 zisizosahihi au za uongo zenye thamani ya Sh 133, 000,000 zikiwa zimetolewa kutoka kwenye mashine ya kieletroniki yenye namba 03TZ843040152 mali ya Africa Harmony Industry and Trade Ltd na mashine nyingine za kieletroniki 13 kampuni ya INCOTEXT zikisadikika kuwa za wizi au zimepatikana kinyume cha sheria na mashine hizo zilihodhiwa.

Pia, alidai katika kumhoji mshtakiwa Mhavile alimtaja mshtakiwa Kagale kuwa ndiye mwenye mashine iliyotumika kutoa risiti hizo zisizo sahihi alizokutwa nazo.

"Kutokana na maelezo ya Mhavile juhudi za kumtafuta Kagale zilianza na Julai 19, 2023 wapelelezi walipokea taarifa kutoka kwa msiri kuwa Kagale ana rafiki wa kike aitwaye Salma Ndauka ambaye ni mshtakiwa namba nne," aliendelea kudai.

Julai 19, 2023, alidai alikamatwa na katika upekuzi alikutwa na mashine 10 za kieletroniki aina ya INCOTEX ambapo mashine nane ndizo zilitambulika namba zake na mashine mbili hazikutambulika kwani zilifutika na kwamba mashine hizo zilihodhiwa.

Vilevile, alidai kuwa wakati wa kumhoji mshitakiwa Ndauka alimtaja pia, Kagale kuwa ndiye mwenye mashine hizo.

Wakili Tumpale alidai kuwa Januari 16, mwaka huu, Kagale alikamatwa na katika mahojiano alikiri kuwa mashine za kieletroniki alizokutwa nazo mshtakiwa Ndauka ni za kwake na alikiri kutumia mashine hizo kutoa risiti mbalimbali za kieletroniki zisizosahihi.

Kwa mujibu wa Tumpale, uchunguzi ulibaini kuwa mashine yenye yenye namba 03TZ443024331 mali ya Kampuni ya Oceanic Cachet katika kipindi cha kati ya Aprili, 2023 na Julai, 2023 ilitumika kutoa risiti ya za uongo au zisizo sahihi za Sh 1,932,096,214.28 na kutokana na kiasi hicho jumla ya kiasi cha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Sh 294,726,540.37 hakikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alidai mashine yenye namba 03TZ442007272 mali ya Tabisco Enterprises ltd katika kipindi cha kati ya Aprili, 2023 na Juni, 2023 ilitumika kutoa risiti ya za uongo au zisizo sahihi za Sh. 2,375,310,754.61 na kwamba kiasi cha Sh 373,537,333.9 kama VAT hakikuwasilishwa TRA.

Pia, alidai mashine yenye namba 03TZ843040152 mali ya Africa Harmony lndusry and Trade Ltd katika kipindi cha kati ya Mei, 2023 na Juni, 2023 ilitumika kutoa risiti ya za uongo au zisizo sahihi zenye jumla ya Sh. 1,929240,063.00 na Sh. 303,713,897.37 kama VAT hakikuwasilishwa TRA.

Kutokana na hali hiyo, alidai kuwa washtakiwa waliisababishia hasara ya Sh. 971,977,772.32 na kwamba walipotosha mfumo na Kamishna Mkuu wa kwa kuonesha kuwa Kampuni ya Oceanic Cachet imefanya mauzo ya Sh 1,932,096,214.28, Kampuni ya Tabisco Enterprises ltd imefanya mauzo ya Sh 2,375,310,754.61 na Kampuni ya Africa Harmony lndusry and Trade ltd imefanya mauzo ya Sh 1,929240,063.00.

Wakili Tumpale alidai wakati wa uchunguzi ilibainika zaidi kuwa watuhumiwa wote wanne walikuwa wakiongoza na kuratibu genge la uhalifu wa makosa mbalimbali ambayo ni kutoa risiti zisizo sahihi, kutumia mashine za kieletroniki kwa namna ya kuupotosha mfumo au Kamishna Mkuu wa TRA, kukwepa kodi kinyume na sheria, kuisababishia hasara TRA na kutakatisha fedha.

Alidai kuwa, washitakiwa wote walifikishwa mahakama hiyo kujibu mashitaka yanayowakabili.

Baada ya kusomewa hoja za awali, washitakiwa wote walikiri majina yao, maeneo wanayoishi na kufikishwa mahakamani hata hivyo, walikana mashtaka yote.

Mshtakiwa Mhavile alikana dini iliyoandikwa kwamba ni Mkristo akidai yeye ni Mwislamu, pia alikana kuwa fundi wa mashine za kielektroniki na kueleza kuwa yeye ni msambazaji wa mashine hizo.

Hakimu Kuppa aliahirisha shauri hilo hadi Septemba 24, mwaka huu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Washtakiwa walirudishwa rumande kwa kuwa mashitaka yanayowakabili hayana dhamana.

# Aweso ajivunia uwapo kiwanda mabomba

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso amesema uwapo wa kiwanda cha mabomba ya maji mkoani Simiyu, kutarahisisha utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kuelekea mikoa mbalimbali nchini.

Kabla ya kiwanda hicho cha Moli Oil Mills kinachomilikiwa na mwekezaji mzawa, Emmanuel Silanga, serikali ilikuwa inafuata mabomba hayo Dar es Salaam kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Aweso aliyasema hayo jana mkoani Simiyu, katika ziara yake aliyotembelea kiwanda hicho, kilichopo mtaa wa Majahida katika Wilaya ya Bariadi.

"Uwapo wa kiwanda hiki, utasaidia utekelezaji wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria. Katika mradi huo, yatatumika mabomba haya, hivyo mwekezaji ametumia fursa kwa wakati sahihi," alisema.

Sambamba na hilo, alieleza kufurahishwa na hatua ya mwekezaji huyo kujenga kiwanda hicho katika Mkoa wa Simiyu, kwa kuwa imezoeleka wengi wangekimbilia kuwekeza Dar es Salaam.

"Angeweza kujenga kiwanda hicho jijini Dar es Salaam ama kwingine, lakini kaamua kuwa mzalendo kwa kukumbuka nyumbani kwanza, hivyo ajira zitamwagika kwa wingi kwani ni kiwanda cha kisasa," alisema.


Mbali na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya utekelezaji wa miradi ya maji, Aweso alisema uwepo wa kiwanda hicho utaibua fursa za ajira kwa vijana wa mkoa huo.

Fursa hizo za ajira, kwa mujibu wa waziri huyo, zitakuza maendeleo ya wananchi na jamii kwa ujumla, akisisitiza uwekezaji huo ni matokeo ya kuboreshwa kwa mazingira ya biashara kunakofanywa na serikali.

"Rais wetu (Samia Suluhu Hassan) ameweka wepesi kwa wawekezaji kufanya kazi kwa moyo na kujituma kwa bidii," alisema.

Mwekezaji wa kiwanda, Silanga, alisema uwezo wake wa kuwekeza katika mradi huo umetokana na mazingira mazuri ya biashara nchini.

Silanga ambaye pia ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Simiyu, alisema wawekezaji wakiwemo wazawa wanapata moyo na nguvu ya kuwekeza kutokana na mazingira hayo.



Waziri wa Maji, Juma Aweso (wa pili kulia), akimsikiliza Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, mkoa wa Simiyu, Emmanuel Silanga (kushoto), kuhusu uzalishaji wa mabomba kwa ajili ya miundombinu ya maji kwenye kiwanda cha Moli Oils Mills, wilayani Bariadi, mkoani humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WMA yahimiza ushirikiano na sekta binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Alban Kihulla, ametoa wito kwa taasisi, asasi na mashirika binafsi kuimarisha ushirikiano na wakala hiyo katika masuala yanayohusu vipimo kwa nyanja za biashara, afya, usalama na mazingira.

Kihulla alitoa wito huo juzi alipokuwa akizungumza na wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari katika mkutano ulioandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina, jijini Dar es Salaam.

Akitoa taarifa ya utendaji kazi, majukumu na mafanikio ya WMA, alisema kuna maeneo 17 ambayo sekta binafsi inaweza kushirikiana na WMA ili kuongeza tija katika sekta ya vipimo.

Kihula akitaja baadhi ya maeneo hayo ya kivipimo kuwa ni ukaguzi na uhakiki wa mizani, uhakiki wa mitambo ya gesi, dira za maji zilizoko kwenye matumizi, mashine za michezo ya kubahatisha na lifti za majengo.

Kuhusu sheria inayoipa mamlaka WMA kutekeleza majukumu yake, Kihula alisema sheria hiyo ambayo msingi wake hasa ni vitabu vitakatifu vya dini, yaani Quran na Biblia, ni ya Usimamizi wa Vipimo Sura Namba 245 na 340 ya Mwaka 2002 ambayo inawatambua maafisa vipimo kama wakaguzi wanapotekeleza majukumu ya ukaguzi na uhakiki wa vipimo.

Alibainisha kuwa jukumu kubwa la WMA ni kuilinda jamii ili kuepukana na madhara yatokanayo na matokeo ya upimaji usio sahihi katika biashara ambapo WMA inawajibika kukagua sehemu za biashara kama vile maduka ya kuuzia bidhaa mbalimbali, viwanda, maduka ya vifaa vya ujenzi, vituo vya kujazia mafuta na sehemu nyinginezo.

"Tunasisitiza kila mara kwa wananchi kuwa, ukihisi kwamba umepimiwa visivyo sahihi katika sehemu uliyoenda kupata huduma, ni jukumu lako kutoa taarifa ili wataalamu wetu wakafanye uchunguzi eneo hilo," alisema.

Mtendaji huyo mkuu aliongeza kuwa WMA inawajibika kuhakiki mzunguko mzima wa mafuta kuanzia yanapoingia nchini kupitia bandari, uhakiki wa matangi na maghala ya kuhifadhia mafuta na wakala hufanya shughuli hizo kupitia kitengo maalum cha bandari.

Sambvamba na hayo, Kihulla alibainisha kwamba WMA ina mpango wa kuingia kwenye maeneo mapya ya uhakiki wa vipimo kama vile uhakiki wa gharama za vifurushi vya muda wa maongezi na mashine za michezo ya kubashiri.

Mpango mwingine, alisema ni kutoa elimu kwa wananchi na wadau wa vipimo kuhusiana na matakwa ya sheria ya vipimo, kuendelea kuboresha mifumo ya utendaji kazi pamoja na kuwajengea uwezo zaidi wataalamu wake ikiwa ni kuwapa mafunzo zaidi na ununuzi wa vifaa vya kisasa.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile ameipongeza WMA kutokana na utendaji kazi wake na ameahidi ushirikiano wa vyombo vya habari na Wakala hiyo ili kuhakikisha elimu ya matumizi sahihi ya vipimo inawafikia wananchi kwa ukubwa wake.

"WMA mna nafasi ya kuufikia umma wa watanzania kwa kutumia vyombo vya habari kwenye kampeni hizi za kivipimo, elimu inahitajika sana, wananchi wanatakiwa kufahamu kwamba wanapaswa kuwa makini wanapokwenda kupata huduma mbalimbali, hii itachagiza maendeleo katika taifa letu" alisema.

## Wanawake Dar kupewa mitungi 10,000 gesi bure

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema hivi karibuni Mkoa utagawa mitungi 10,000 ya gesi kwa wanawake kama mkakati wa kuondokana na matumizi ya mkaa na kuni.

Aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kongamano la matumizi ya nishati safi ya kupikia katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam ambapo mitungi ya gesi 1,000 iliyotolewa na Lake Gas iligawiwa kwa wanawake wa wilaya za Mkoa huo.

Aliziagiza taasisi za serikali mkoani hapa kuchangia mitungi 300 ya gesi kabla ya mwisho wa mwezi huu ambayo itagawiwa kwa wanawake kama mpango wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alizitaka taasisi hizo kujipanga na kuhakikisha zimetekeleza agizo hilo haraka kwani wiki mbili zijazo mkoa wa Dar es Salaam utazindua ugawaji mwingine wa mitungi 10,000 kwa wanawake wa Mkoa huo.

"Hata hapa naziona taasisi nyingi za serikali, Katibu Tawala wa Mkoa uko hapa nakuagiza waandikie barua taasisi zote za serikali wachangie mitungi ya gesi kwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambayo itagawiwa kwa wanawake kama mkakati wa kulinda afya zao dhidi ya matumizi ya mkaa na kuni," alisema

Alisema ameagiza taasisi hizo kutoa mitungi ya gesi kwasababu mkakati wa utekelezaji wa mpango wa matumizi ya nishati safi kwa kupikia lazima ufungamane na taasisi mbalimbali za serikali.

Chalamila alisema kaulimbiu inayotumika kwenye kampeni ya matumizi ya nishati safi ni jali fya, pika kijanja, tumia nishati safi, okoa mazingira kiuchumi.

Alisema lengo la mkakati huo ni kuwaondoa wanawake nchini kwenye matumizi ya mkaa na kuni kupika kwani nishati hiyo imeonyesha madhara mengi kiafya.

"Lazima tutambue na kuwathamini wadau wetu wa nishati safi ambao wamekuwa wakijitolea kwa hali na mali kuhakikisha mkakati huu unafanikiwa wakiwemo watu wa Lake Gas ambao kila tunapokuwa na jambo wamekuwa wakitusaidia," alisema.

Chalamila alisema tarehe 23 kutakuwa na tamasha la mapishi kwa kutumia nishati safi na watu 1,000 watakaokuwa wa kwanza kufika kwenye tamasha hilo kila mmoja atapewa shilingi 20,000.

"Mama lishe, wapishi na wachoma nyama wote waje kwa wingi kwenye tamasha hilo namimi nitawaletea wateja wengi sana kama biashara watafanya ya kutosha waje wasihofie kukosa wateja kwasababu watakuwepo wa kutosha," alisema.

Alimtaka katibu tawala kuwaandikia viongozi wa vyuo vikuu na taasisi mbalimbali za elimu ya juu kuchangia angalau mitungi miamoja hadi miambili.

"Kesho nitatangaza tutakutana eneo gani kwa hiyo wewe kama ni mama lishe njoo upike, kama wewe unachoma nyama njoo uchome nyama, usiwe na hofu kwamba vyakula vyako vitakosa wateja watakuwepo kwa wingi sana na vyote vitaisha," alisema



# Wanafunzi waondokana na kikwazo kukatisha masomo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAFUNZI wa Kata ya Hombolo jijini Dodoma, wameondokana na vikwazo vinavyowasababisha kukatiza masomo baada ya kujengwa kwa shule ya sekondari mpya iliyopo mtaa wa Mkoyo.

Akizindua shule hiyo jana, Mbunge wa Dodoma Mjini na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema wanafunzi hao walikuwa wakitembea umbali wa kilomita 15 kufuata elimu hali iliyokuwa ikisababisha wengine kukatiza masomo kwa utoro na mimba.

"Nimejisikia furaha ile ndoto yetu ya kuwapunguzia mwendo wanafunzi wa sekondari kutembea kilomita 15 hatimaye tumeitimiza, Shule hii imeanzisha ujenzi wake wa madarasa ya awali na baadae kupata ushirikiano wa serikali kupitia Halmashauri ya Jiji Dodoma.

"Niliahidi kwamba serikali sikivu chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan itasikia hitaji hili na hivyo kuwaunga mkono ili kuwanusuru watoto kutembea kilomita 15 kufuata Shule Sekondari ya Hombolo Bwawani," alisema.

Alisema watoto wengi wa kike walishindwa kumaliza masomo yao kwa kupata ujauzito kutokana na vishawishi mbalimbali kwa umbali waliokuwa wanatembea.

"Nilikuja hapa pakiwa pori,tukachimba msingi pamoja na kuanza ujenzi,naishukuru serikali chini ya RaisSamia kupitia Halmashauri ya Jiji kutuunga mkono kwa kuongeza madarasa mawili na pia tunatarajia kujenga madarasa mawili mengine," alisema.

Mavunde aliahidi kusaidia kuingiza umeme shuleni pamoja na kuwaletea kompyuta na mashine ya kudurufu, kuchangia malipo ya walimu wanaojitolea na kununua pikipiki mbili watakazozitumia kama kitega uchumi cha kukidhi baadhi ya mahitaji.

Naye, Diwani wa Hombolo Assedi Ndajilo, alimshukuru Mavunde kwa uanzishaji wa ujenzi wa shule hiyo na kuwataka wazazi kuhakikisha wanawasimamia vizuri wanafunzi ili shule ilete matokeo tarajiwa.

Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, alisema jiji hilo litaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Mbunge na kuahidi upatikanaji wa maabara shuleni hapo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Dodoma, Charles Mamba, alisema ujenzi wa shule hiyo ni utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM ya kusogeza huduma kwa wananchi.

# TAKUKURU yashangaa watumishi kulalamikia rushwa maeneo ya kazi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imesema watendaji walioko ndani ya serikali hawatakiwi kulalamika uwapo wa vitendo vya rushwa badala yake wachukue hatua za kuzuia kwenye maeneo yao ya kazi.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Petro Horombe, aliyasema hayo juzi baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera,Bunge na Uratibu, William Lukuvi, kutembelea banda la taasisi hiyo kwenye maonesho ya saba ya kitaifa ya Mifuko ya Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yanayofanyika mjini hapa.

Horombe alisema katika dhana ya mapambano dhidi ya rushwa, kila mtendaji wa kata na kijiji kwenye eneo lake ndiye kamanda namba moja katika mapambano dhidi ya rushwa.

Alisema mtendaji wa kata ni mlinzi wa amani katika eneo lake na rushwa ni uhalifu na kosa la jinai, hivyo watendaji wanao wajibu wa kukomesha vitendo hivyo kwenye maeneo yao.

"Mfano kuna miradi inasuasua kata ya Isuna, Manispaa ya Singida na pengine kuna harufu ya rushwa, mtendaji anatakiwa kutoa taarifa TAKUKURU," alisema.

Alisema TAKUKURU imeshiriki maonesho hayo ili kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi ili kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa hususani kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, 2024 na uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani.

Alisema TAKUKURU inatoa elimu hiyo katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa kutokananawananchininguzo muhimu katika kuzuia vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi.

Horombe alisema wananchi wakijiepusha na vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi, nchi itakuwa na uchaguzi mzuri usiokuwa na rushwa jambo ambalo linawezekana kabisa.

Alisema hivi karibuni TAKUKURU iliendesha mafunzo kwa ajili ya kuhamasisha jamii kujiepusha na vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi ambayo ilifanyika Julai 31, 2024 katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa iliyowashirikisha viongozi wa vyama vya siasa, dini na asasi za kiraia.

Katika mafunzo hayo, alisema kuliwekwa azimio la pamoja la kushirikiana katika kuhamasisha jamii kushiriki katika kudhibiti na kuzuia vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi.

Alisema wananchi wanapoelimika na kuhamasika kuichukia rushwa, kuikemea, kuikataa na kutoa taarifa ya rushwa TAKUKURU, vitendo hivyo vitaondoka kabisa.




Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Omari (kushoto), akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa wadau wa uchaguzi Mkoa wa Singida jana, kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unaotarajiwa kufanyika mkoani humo kuanzia Septemba 25 hadi Oktoba mosi mwaka huu. **PICHA: INEC**

# NGO zaaswa elimu dawa za kulevya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MASHIRIKA Yasiyo ya Kiserikali yametakiwa kuendesha kampeni ya kufikia jamii kutoa elimu kuhusu hatari ya matumizi ya dawa za kulevya ili kuondokana na hali hiyo.

Aidha, balozi mbalimbali nchini zimeombwa kufungua milango kuona namna ya kusaidiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) pamoja na serikali katika kukabiliana na dawa za kulevya.

Kamishna Msaidizi wa Mamlaka hiyo Kanda ya Kati, Mzee Kasuwi, alitoa wito juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza kuhusu nafasi ya asasi za kiraia kwenye mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Alisema mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa yakifanya kazi kushawishi sera ya dawa za kulevya na kutetea marekebisho hivyo wanaweza kufanya kampeni ya mikakati ya kupunguza madhara au mabadiliko ya sheria ili kushughulikia vyema masuala ya afya ya umma na jamii.

"Mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kutoa huduma za usaidizi kwa familia zinazohusika na uraibu wa dawa za kulevya kwa kuhusisha ushauri,nyenzo za elimu na vikundi vya usaidizi ili kusaidia familia kukabiliana na athari za matumizi ya dawa hizo," alisema.

Pia alisema mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kufanya utafiti kuhusu mwelekeo wa matumizi ya dawa za kulevya,ufanisi wa afua tofauti na athari pana zaizi za masuala yanayohusiana na dawa hizo.

Aidha, Kamishna Kasuwi alisema DCEA inashirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika kutoa elimu kwa jamii na kutoa wito kwa asasi 6,771 pamoja na wananchi kushiriki kutoa taarifa za dawa za kulevya.

kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, na uchaguzi mkuu wa mwakani, Kamishna Kasuwi aliyaomba mashirika hayo kushirikiana na serikali katika kutoa elimu ya uchaguzi.

"Tuna uchaguzi wa serikali za mitaa, hivyo niwaombe asasi za kiraia msiache jukumu hili muhimu kwa nchi yetu,mamlaka pamoja na wadau wote tushirikiane katika kuibeba ajenda hii muhimu ambayo kwa sasa tunayo nchini na tuhakikishe tunaifanikisha," alisema.



# SMZ yatoa sababu kuchelewa umeme Nungwi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imesema Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) limeshindwa kuwapatia umeme wananchi wa Nungwi kwa wakati baada ya kuchelewa kwa kuwasili kwa vifaa vya kuunganisha umeme, zikiwamo nguzo.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Zawadi Nassor Amour, alisema jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Nungwi, Abdalla Abbas.

Mwakilishi huyo alitaka kujua lini ufanisi katika utoaji wa huduma hiyo utarejeshwa kutokana na baadhi ya watendaji wa shirika hilo kulalamikiwa kurudisha nyuma jitihada za kuwaunganishia wananchi umeme.

Je, ni lini mtindo huu wa kuchelewesha kutoa huduma kwa wakati na ufanisi utarekebishwa?" alihoji.

Naibu Waziri aliwaomba radhi wananchi wa Nungwi na kusema kwa sasa nguzo na vifaa vinavyohitajika kuwaunganishia huduma ya umeme vipo na kazi hiyo inakwenda kwa kasi kubwa, ili wote walioomba kuunganishiwa wawe wamepata huduma hiyo kabla ya mwisho wa Oktoba, mwaka huu.

"Mheshimwa Mwakilishi atakuwa shahidi mbele ya Baraza lako tukufu kwa kazi inayofanyika Nungwi kwa sasa ya kuwaunganishia wananchi umeme kwa wale walioomba," alisema.

Pia alisema mradi wa jamii (kisima) wa Jimbo la Nungwi kwa taarifa alizonazo ni kuwa, miradi ya maji imefikishiwa huduma ya umeme na iko ambayo haijaunganishwa lakini ila umeme ushafika.

"Shirika linasuburi wenye miradi kukamilisha taratibu zilizobaki ikiwa ni pamoja na kulipia mita na baada ya kukamilisha taratibu ndani ya masaa 24, visima hivyo vitaunganishiwa huduma ya umeme," alisema.

**Alisema taasisi hizo zimekuwa zikiunga mkono jitihada za ZAECA za kujiimarisha kiutendaji kwa kuipatia mafunzo ya kitaalamu na wataalamu katika nyanja mbalimbali za kuzuia na kupambana na rushwa.**

Naye Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema, serikali kupitia Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) imekuwa ikinufaika katika miradi mbalimbali ya kikanda na kimataifa inayofadhiliwa na jumuiya ya kimataifa ikiwamo Basel Institute on Governance na Ubalozi wa Uingereza.

Alisema taasisi hizo zimekuwa zikiunga mkono jitihada za ZAECA za kujiimarisha kiutendaji kwa kuipatia mafunzo ya kitaalamu na wataalamu katika nyanja mbalimbali za kuzuia na kupambana na rushwa.

Pia alsiema ZAECA na taasisi zingine za haki jinai zimeshaanza utekelezaji wa mradi wa kujengewa uwezo unaodhaminiwa na Ubalozi wa Uingereza na Ubalozi wa Uswisi ambao unatoa msaada wa mafunzo na vitendea kazi



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kulia), akiteta jambo na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Nassor Jazira, wakati wa kikao cha uwasilishaji wa Muswada wa kufuta Sheria ya Mtoto Namba 6 ya mwaka 2011, katika Wizara hiyo, Kinazini, Unguja mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yakiri uhaba walimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema inatambua kuwepo kwa uhaba wa walimu kisiwani Pemba.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Ali Hussein Gulamu, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mtambwe, Muhammed Ali Suleiman, aliyetaka kujua seriali ina mipango ipi ya kuwapeleka walimu katika shule zenye uhaba wa watumishi hao.

Alisema wizara imetangaza nafasi za ajira ya walimu na kwa sasa walioomba nafasi hizo wamefanya usaili na hatua za kukamilisha mchakato wa ajira ziaendelea.

Naibu Waziri alisema wizara inaahidi kupeleka walimu katika shule zenye uhitaji ikiwamo Uondwe kisiwani Pemba na minogoni mwa sababu inayofanya walimu wanaoajiriwa katika shule hiyo kutokukaa na kuhamishiwa shule ziengine ni kutokea kwa dharura kwa baadhi ya shule jirani ambazo zina uhaba mkubwa zaidi wa walimu.

Aidha, alisema serikali inapokea maoni ya mwakilishi huyo ndiyo maana iliamua kuajiri walimu katika maeneo tengefu yakiwamo ya visiwa vidogo vilivyoko Unguja na Pemba.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema wizara inawauzia wakulima pembejeo za mbolea na dawa kwa bei ya ruzuku ya asilimia 50 ya bei ya soko, ili kuwapatia unafuu.

Alisema kwa mwaka 2023, serikali haikutoa pembejeo za ruzuku kwa wakulima kama ilivyo kawaida, ingawaje walipata huduma hiyo kutoka kwa wafanyabiashara binafsi.

"Kwa mwaka wa fedha 2024/25, serikali imetenga Sh. bilioni 5.5 kwa ajili ya kununua mbolea, mbegu na kuwapatia wakulima kwa bei ya ruzuku ambazo zinatarajiwa kuuzwa kwa matumizi ya msimu ujao" alisema Shamata.

# Wizara yaunga mkono uwezeshaji vijana kupitia mafunzo ya ufundi

**Na Mwnadishi Wetu**

SERIKALI imesema inaunga mkono juhudi za serikali mbili za kuwawezesha vijana kujifunza stadi za kazi ambazo zitawajengea msingi mzuri wa maisha na kujiajiri kupitia vyuo vya amali.

Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Zawadi Nassor Amour, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wahitimu wa mafunzo ya stadi za kazi katika sherehe za mahafali ya 10 ya Chuo cha Mafunzo ya Amali cha Vitongoji, Chake Chake, kisiwani Pemba.

Alisema uwekezaji wa fedha unaotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendesha vyuo vya mafunzo ya amali na kujenga majengo ya kisasa yakiwa na vifaa kamili, una lengo la kuwawezesha vijana kupata elimu ya mafunzo ya vitendo, kazi za mikono na kujiajiri.

Zawazi alisema hayo ndiyo malengo yanayotokana na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuona kundi la vijana linajiajiri katika kazi za mikono na kuondokana na mawazo ya kuajiriwa.

Pia aliwataka wahitimu hao kuyathamini mafunzo waliyoyapata na kuyafanyia kazi kwa ajili ya kuleta mageuzi makubwa ya maisha yao na kujitegemea.

"Hayo ndiyo malengo ya kuanzishwa kwa vyuo vya amali Zanzibar na ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 kuona kwamba vijana wanapata mafunzo ya stadi za maisha kwa ajili ya kujitegemea na kujiajiri," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Vyuo vya Amali, Dk. Bakari Ali Silima, alisema fursa ya kuwasomesha vijana stadi za kazi katika chuo hicho yamezingatia fursa sawa kwa makundi yote. Wahitimu 131 wamemaliza masomo yao katika fani mbalimbali kwenye chuo hicho.

"Vyuo vya mafunzo ya amali lengo lake kubwa ni kuleta mageuzi ya vijana kutoka mawazo ya kuajiriwa serikali hadi kujiajiri baada ya kupata stadi za kazi na ufundi," alisema.

Mkuu wa Chuo cha Mafunzo Amali, Biubwa Mohamed Mselem, alisema mafanikio makubwa yamepatikana kwa wahitimu wa chuo hicho wengine kuajiriwa serikalini na sekta binafsi baada ya kupata ufundi katika fani mbalimbali.

Pia aliitaka Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kuwekeza zaidi na kulipatia ufumbuzi tatizo la ukosefu wa vifaa vya kufundishia vijana masomo ya vitendo.

Alisema chuo hicho ambacho kilianzishwa mwaka 2012, kimetoa wahitimu 1,000 katika fani mbalimbali na kuingia katika soko la ajira ikiwamo sekta binafsi.

"Changamoto kubwa ambazo zinatakiwa kupatiwa ufumbuzi na Mamlaka ya Vyuo vya Amali ni upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya kufundishia kazi za mikono" alisema.

Ali Hamadi Issa, mmoja wa wahitimu wa chuo hicho alisema amefaidika na kupata mafunzo katika sekta ya fundi umeme ambapo matarajio yake ni kujiajiri katika sekta binafsi.

Vijana 95 wamehitimu katika mafunzo ya muda mrefu wakati vijana 36 wamehitimu mafunzo ya muda mfupi. Kati ya hao vijana 16 ni wenye mahitaji maalumu na wamekabidhiwa vyeti.



**PROF. J**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

JUMAMOSI SEPTEMBA 14, 2024

BT
BURUDANI TELE



# ANJELLA USIPOTOKE

WIKI hii msanii wa muziki wa Bongo Fleva, Anjella amejikuta akikabiliana na Mwijaku kutokana na madai ya kutumika vibaya na wanamuziki maarufu Diamond na Nandy.

Mwijaku alitoa tuhuma hizo akidai Diamond na Nandy ambao wamemualika Anjella kushiriki katika matamasha yao ya muziki, wanafaa kumshukuru kwanza Harmonize kwa kumleta Anjella kwenye mwanga.

Anjella naye alijitokeza na kumtaka Mwijaku kuacha kumwingilia kwani kufanya hivyo sawa na kumharibia riziki yake.

Anjella alifafanua kuwa anaheshimu kwa kiasi kikubwa mchango wa Harmonize, lakini hilo lisimfanye kuwakumbusha kila mtu anayetaka kumsaidia, kwani tayari ukurasa wa Konde Gang umeshafungwa.

Hata hivyo, wadau wa muziki wameeleza kwamba Anjella yuko sahihi kumkumbusha Mwijaku, kuwa kila anachokiona ni lazima akitolee maoni kwani wakati mwingine kunajitokeza athari.

Shukuru Mbwembo, amesema kwamba Anjella kwa sasa anajitafuta baada ya kuondoka Kond Gang, hivyo hakuna sababu ya kutafutiwa marafiki wa kumsaidia.

"Nakumbuka Anjella baada ya kutoka lebo ya Harmonize, alionekana kuyumba sana mpaka mwaka huu jina lake lililopanza kutajwa tena. Alichokifanya kumkosoa Mwijaku ni sahihi kwa sababu hawezi kumtafutia marafiki," amesema Mbwembo.

Amesema ni muhimu kwa Anjella kutosikiliza maneno ya watu na kuacha kujibu kila kitu anachokiona katika mitandao ya kijamii kwani kwa kufanya hivyo kutamfanya kuondoka katika njia.

BASI SAWA

## Dr Cheni kaanza kichovu



MWIGIZAJI wa filamu za Bongo Muvi, Dr Cheni, amesema ameingia katika tasnia hiyo kwa bahati pekee.

Amesema anakumbuka siku moja akiwa katika ufukwe wa Coco, alikutana wa watu wakichukua filamu ndipo na yeye aliamua kukatiza nyuma ya wasanii kitu ambacho kilimvutia mwongozaji.

"Wakati walipomaliza kuandaa kamera wanataka kuanza kurekodi, mimi nikakatiza katikati, mwongozaji akasema 'cut' akaniambia wewe jamaa umekatiza vizuri sana, unaweza kurudia hiyo? nikarudia na pale wakaniomba niende kwenye mazoezi yao ya kuigiza," amesema dr Cheni.

## Wema Sepetu unamuona kivingine



MWIGIZAJI mkonwe wa filamu, Wema Sepetu, amesema kuanzia sasa mashabiki wake watarajie kumuona akivaa suti za Rais Samia Suluhu Hassan.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Wema amesema uamuzi wake ni kumuunga mkono kiongozi huyo na kuwahamasisha wanawake kuvaa nguo za aina hiyo.

"Mimi ni mtoto wa Mama Samia nami nikasema jambo la Mama yangu haliwezi kunipita nimeamua kuonyesha ni jinsi gani vazi la Rais wetu ni la kipekee na zuri sana," ameandika Wema.




## OMBI KWA PROFESA JAY...

MASHABIKI wa muziki wa kizazi kipya wamekuwa na furaha baada ya msanii mkongwe Profesa Jay, kueleza kwa sasa yuko kamili baada ya muda mrefu kupambana na afya yake.

Kupitia ukurasa wake wa Istagram, Profesa Jay, amesema yuko gado kwa mapambano na kumshukuru Mungu kwa kumpa zawadi ya uzima na kumlinda siku zote.

Baadhi ya mashabiki walichangia maoni katika chapisho hilo kwa kumuomba afanye ngoma ambayo itakuwa zawadi kwao kutokana na kumsubiri kwa muda mrefu wakati akipambania maisha yake.





## Shamsa, Mlilo msiwarushe roho

WAIGIZAJI maarufu wa Bongo Muvi, Shamsa Ford na Mlilo, wameibua gumzo baada ya kuweka video mtandaoni wakionekana wakipigana mabusu.

Video hiyo iliyochapishwa kwenye ukurasa wa Instagram, inawaonyesha wanandoa hao wakisikiliza wimbo wa Michael Jackson, huku Mlilo akionekana kupagawa na kumpiga mabusu mfululizo Shamsa.

Mchangiaji mmoja, Miss Reeny, alishindwa kujizuia na kuwauliza wanawezaje kupendana hadi wanaanza kufanana ikiwa yeye ana wiki moja tu keshapewa onyo.

## MADEMU WA KISAUZI WALIOTIKISA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

TANGU enzi za ubaguzi wa rangi, nchini Afrika Kusini kumekuwa na wanamuziki wengi mahiri kubahatika kutamba ndani na nje ya nchi hiyo.

Kwa bahati ni kwamba wanamuziki wengi mastaa Sauzi ni wenye weusi, ambao walifanya kazi kubwa tangu enzi za kudai uhuru hadi ulipopatikana. Wakaendelea na maisha ya muziki, lakini wakajitokeza wengi wazuri zaidi.

Kifupi tu ni kwanza Sauzi haijawahi kukaukiwa na wanamuziki mahiri na wenye viwango vya hali ya juu.

Hapa nchi mbali na kuwapokea wapigania uhuru, lakini pia ilipokea baadhi ya wanamuziki wakawa wanapiga bendi mbalimbali kabla ya nchi yao kupata uhuru na kuondoka.

Leo hii tunawaangalia wanamuziki wa kike tu ambao walipata kutamba Afrika nzima, wakijipatia mashabiki wengi nchini Tanzania kutokana na nyimbo zao.

### Miriam Makeba

Huyu anaitwa mama Afrika. Alizaliwa mwaka 1932 na kufariki dunia 2008 bado akiwa bdao mwanamuziki. Ni mmoja wa wanamuziki maarufu sana si Afrika tu bali dunia nzima. Alianza kuimba nyimbo zake wakati ule wa ubaguzi wa rangi na zikavuma sana, zikawa maarufu hadi leo hii.

Baadhi ya nyimbo zilizompatia umaarufu mkubwa ni kama 'Patapata', 'Hapo Zamani', 'Malaika', "Welela', 'Soweto Blues' na nyingine nyingi ambazo zilikuwa na mashabiki wengi nchini.

### Doroth Masuka

Unaweza ukasema kama huyu ni [illegible]cha ya Miriam Makeba. Naye alizirudia nyimbo za [illegible]atapata' na 'Hapo Zamani'. Pia kuna utata kwani inasemekana huenda Doroth ndiye mtunzi halisi ya wimbo wa 'Hapo Zamani' Ana uraia wa Zimbabwe na Afrika Kusini pia. Alishawahi kuja nchini miaka ya 1960 na kupigia bendi mbalimbali nchini, akarekodi nyimbo mbili kwa kiswahili kama 'Kunguni' na 'Viongozi Afrika'. Alirejea Sauzi na kuendelea na mambo yake ya muziki akirekodi nyimbo mbalimbali hadi alipofariki nchini Afrika Kusini mwaka 2019.

### Yvonne Chakachaka

Kizazi cha miaka ya 1980 wanam[illegible]mbuka mwanamuziki huyu kwani ndiyo kipindi chao cha utoto wakati nyimbo zake zinazuma.

Umaarufu wake ulianza katikati ya miaka ya 1980 alipotoa albamu yake iitwayo 'Thank You Mr DJ' ya mwaka 1987 ambayo si tu kwamba ilimtoa ikiwa pia na wimbo mwingine maarufu 'Umqombothi', lakini ndiyo kama vile alifungulia maji kwenye koki.

Baada ya hapo alianza kutoa ngoma nfululizo kama vile 'Sangona', 'Bombani', 'I Cry For Freedon' na nyingine nyingi.

### Brenda Fassie

Mwanamuziki huyu aliyezaliwa mwak[illegible] 1964 na kufariki 2004 alikuwa mmoja wa wanamuziki wa kike wa Sauzi waliopendwa sana nchini Tanzania.

Na hasa alipotoa ngoma yake ya 'Vulindlela' ambayo ilikamata sana Bongo kiasi cha yeye mwenyewe kuja nchini na kufanya maonyesha kadhaa. Na alipondoka kurudi kwao alitunga wimbo 'Nakupenda' alioimba kwa lugha ya kiswahili.

### Pamela Nkuta

Ni mwanamuziki ambaye alipata sifa kwa muda mfupi tu hapa nchini kutokana na wimbo wake uitwayo 'Melody' ambao ulikuwa na sauti ya mtoto analia wakati wimbo huo unaanza na yeye mwenyewe kuimba kama vile anambembeleza.

FILAMU

## Baba mwenye nyumba ovyooo

**Na Adam Fungamwango**

"BABA Mwenye Nyumba', ni filamu inayoangazia kwenye jamii za uswahili kule kwenye nyumba za kupanga ambapo wapangaji zaidi ya wawili wanaishi na wenye nyumba humo humo.

Huwa kuna sakata la aina yake, hasa ukutane na mwenye nyumba mkorofi, wapangaji micharuko, au wote kwa pamoja.

Filamu inaanza kuonesha mpangaji kwenye moja kati ya nyumba za uswazi akienda msalani.

Baadaye kidogo anatokea mtu mmoja ambaye anakwenda kugonga humo humo. Kama inavyojulikana uswahilini, choo huwa ni kimoja. Unaweza ukakuta choo kimoja na bafu moja hiyo afadhali. Lakini unaweza kukuta eneo la kujisaidia haja ndogo, kubwa na hata kuoga ni hiyo hiyo moja. Watu inabidi wasubiriane.

Mtu aliyekuja baadaye ni baba mwenye nyumba. Yeye alipoona kuna mtu anagonga ili atoke yeye aingie. Aliyekuwa ndani akagoma na kumwambia mpaka amalize haja zake.

Alipotoka, baba mwenye nyumba akawaka kuwa kwa nini hakuja kumuomba.

Yaani baba mwenye nyumba huyo ana utaratibu ambao ameuweka kwenye nyumba yake kuwa mpangaji yeyote kama anataka kwenda chooni ni lazima amuone kwanza, amuombe ndiyo ampe ruhusa.

Hili limeonekana kuwachosha wapangaji 10 na familia zao waliopanga kwenye nyumba hiyo bila kujua masharti yake.

Siku moja wapangaji wa kike walikuwa wamekaa kibarazani wanamteta baba mwenye nyumba wao ambaye kwanza amekuwa mtu mzima halafu anaishi bila mke, ukichanganya na masharti kibao kwenye nyumba yake kama mganga wa kienyeji, wakawa na wasiwasi labda ni mchawi, au chuma ulete kwani hata kuna baadhi ya pesa wakiweka majumbani mwao zinapotea.

Kwa bahati mbaya sana baba mwenye nyumba akawasikia. Kinamama walidhani ametoka, kumbe alikuwa sehemu amejibanza anawasikiliza.

Akaingia ndani akachukua ndoo ya maji, akatoka nje na kuwamwagia. Kina mama nao kwa hasira wakampakia maneno ya kumchamba, hadi mzee akaona isiwe tabu, akaamua kuwapa notisi wote wahame.

Baadhi ya wapangaji wakasema wala haina shida, na hata kama asingewapa, hata wao wenyewe walipanga kuondoka kodi itakapoisha kwa sababu hawawezi kukaa sehemu ambayo ina mashatri ya ajabu ikiwemo hata ukitaka kwenda msalani lazima upate ruhusa yake.




# Baskermouth kampata mwenza

MCHEKESHAJI kutoka Nigeria, Basketmouth, ameibua gumzo kwenye mitandao ya kijamii baada kuonekana akiangaliana kwa macho ya mahaba na mwamdishi wa habari Victoria Eze.

Basketmouth aliibua mjadala baada ya kuchapisha picha kwenye ukurasa wake wa Instagram akionekana akiwa na Eze wakiangaliana kwa hisia, jambo lilowafanya mashabiki wao kuhoji picha hiyo kama inaendana na ukweli.

Mashabiki hao walimpa pongezi na kueleza furaha yao ya kumwona akiwa na mwanamke mwingine baada ya miaka miwili ya kukaa singo tangu alipomuacha mke wake.





## Do2dtun amponda Tyla

MWIMBAJI kutoka Nigeria, Do2dtun, amemponda msanii kutoka Afrika Kusini, Tyla, kuhusu kuuzungumzia vibaya muziki wa Afrobeat wakati akipokea tuzo za VMA.

Wakati akipokea tuzo hiyo hivi karibuni,Tyla aliusifia muziki wa Amapiano ambao chimbuko lake Afrika Kusini.

"Tumekusikia kuusifia Amapiano lakini wimbo wako "Maji" pia sio amapiano. Ikiwa ulidhani umewekwa kwenye kitengo kisicho sio sahihi, ulipaswa kurudisha tuzo," ameandika kwenye ukurasa wake wa Instagram.

## Toke amkubali D'banj

MWANAHABARI maarufu wa Nigeria, Toke Makinwa, amemtaja mwanamuziki D'Banj kuwa ndiye mwanaume pekee nchini humo aliyempa pesa bila masharti yoyote.

Video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii ilimuonesha mrembo huo akielezea jinsi alivyokumbuka ukarimu aliofanyiwa na mwimbaji huyo kabla ya yeye kuwa maarufu.

Makinwa alisema aliahidiwa kuchangiwa kiasi kikubwa cha fedha na alitimiza ahadi yake bila kutarajia kupewa chochote kutoka kwake.





## Portable kalizua tena

MWANAMUZIKI anayependwa na watu maskini nchini Nigeria, Portable amejikuta katika mzozo baada ya kumtaja mwanamuziki mkongwe wa Afrobeats, Fela Kuti, angeishi muda mrefu zaidi kama angejali kazi yake.

Portable alitoa maoni hayo yenye utata juzi, ambapo alisema mwanamuziki huyo mashuhuri barani Afrika, angeweza kufaidika na kazi yake badala ya kuipigania Nigeria.

"Kama Fela angejali mambo yake kidogo, angeishi muda mrefu zaidi, lakini alikuwa anapigana na serikali. Baada ya Mungu na serikali, hata wazazi wetu ambao walipigana na serikali hiyo hiyo walikuwa na njaa, na mpaka sasa bado tuna njaa," alisema Portable.

## Beyonce kulinda faragha yake

MWANAMUZIKI wa Pop kutoka Marekani, Beyonce, amesema ataendelea kuyaweka maisha yake katika mazingira ya faragha katika kipindi hiki cha digitali.

Mwimbaji huyo ameeleza hayo wakati akihojiwa na jarida la GQ akijikita katika kazi yake ya muziki, biashara na maisha yake.

"Tunaishi katika ulimwengu wa watu kukufikia haraka, nitaendelea kuyaweka maisha yangu faragha na ndivyo nitakuwa siku zinazokuja," amesema Beyonce.





# Waziri asema ufanisi kazini hauhitaji fedha

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, amesema suala la kubadilika kifikra na kuacha kufanya kazi kwa mazoea kwa askari na maofisa waandamizi wa Jeshi la Polisi, kama ilivyoelekezwa na Tume ya Haki Jinai havihitaji fedha, hivyo wanapaswa kuendelea na utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza jana katika Shule ya Polisi Moshi (TPS) na maofisa waandamizi, makamanda wa mikoa na vikosi nchini, alisema utekelezaji wa maagizo hayo unapaswa kusadifu kauli mbiu ya mwaka huu ya mkutano mkuu wa mwaka inayosema, 'huduma bora za kipolisi kwa umma zitapatikana kwa kubadilika kifikra, usimamizi wa sheria na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)'.

Juni 15, mwakah uu, Tume ya Haki Jinai iliwasilisha taarifa yake kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambayo ilionesha maeneo mbalimbali ya kufanyiwa maboresho na mikakati ya kurekebisha utendaji huo.

"Kwenye mikakati hiyo, yako maeneo ambayo yanaweza kufanyiwa maboresho bila kuhitaji fedha na yako mengine yanahitaji fedha. Nielekeze tuendelee kufanya utekelezaji wa maeneo ambayo hayahitaji fedha.

"Mfano suala la kubadilika kifikra na kuepuka utendaji wa mazoea halihitaji fedha,hivyo linawezekana kutekelezeka mapema kama mlivyoweka mikakati ya kuongea na askari kuhusu mabadiliko kwenye mabaraza yenu kila mwezi," alisema.

Miongoni mwa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, ni Jeshi la Polisi kufanyiwa tathmini ya kina itakayowezesha kuwapo maboresho makubwa na kuundwa upya ili kuondoa kasoro za kiutendaji.

Vilevile, ilipendekezwa jeshi hilo libadilishwe kisheria, kimuundo na kifikra na kuwa Polisi Tanzania (National Police Service) ili kutoa taswira kuwa chombo cha kuwahudumia wananchi, kubadilisha mitaala ya mafunzo na mtazamo wa askari ili kutoka katika dhana ya ujeshi kwenda dhana ya kuhudumia wananchi,

Kadhalika, tume ilitaka liboreshe mfumo wa ndani wa kushughulikia malalamiko ya wananchi na liimarishe huduma za intelijensia ya jinai na polisi jamii kwa kuanzisha programu za kuisogeza zaidi kwenye jamii.

Mambo mengine yaliyopendekezwa ni pamoja na Matumizi ya Amri Kuu za Jeshi la Polisi (PGO) kutokana na kubaini kuwa izmetengenezwa pasipo kuzingatia masharti na wigo wa kisheria uliopo katika kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi na sheria nyingine.

Pia ilibainika kuwa miongoni mwa mambo yenye shida kubwa katika PGO ni pamoja na uchunguzi wa vifo vyenye utata, gwaride la utambuzi wa mhalifu, hivyo kutaka PGO yenye GN. Na. 351/2021 inayotumika sasa isitishe matumizi yake na PGO iliyokuwapo awali iendelee kutumika.

Awali, Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, Inspekta jenerali (IGP) Camilus Wambura, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo,alisema Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kufunga mkutano mkuu wa mwaka wa maofisa waandamizi wa Jeshi la Polisi nchini, Septemba 17 mwaka huu katika Shule ya Polisi Moshi (TPS).

## RC aahidi mifuko 1,000 ya saruji makazi ya polisi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ameahidi kutoa mifuko 1,000 ya saruji kwa Shule ya Polisi Tanzania (TPS), kwa ajili ya kukarabati makazi ya askari ambayo ni chakavu na hayavutii kuishi.

Babu amesema serikali ya mkoa huo pamoja na wadau wanaomuunga mkono, watatoa saruji hiyo ili kurejesha makazi hayo katika hali ya kawaida.

Alikuwa akizungumza jana katika shule hiyo, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa mwaka wa maofisa waandamizi wa Polisi nchini.

Mkuu wa mkoa alisema serikali ya mkoa huo, iko tayari pia kuongeza saruji nyingine ili kumalizia mradi huo.

"Nimeshazungumza na Mbunge wa Moshi Mjini (Priscus Tarimo), Mwenyekiti wa CCM Mkoa na RAS (Katibu Tawala wa Mkoa), serikali itatoa mifuko 1,000. Ili kumuunga mkono IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini) ambaye anafanya kazi nzuri," alisema.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camilus Wambura, alisema Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kufunga mkutano mkuu wa mwaka wa maofisa waandamizi wa Jeshi la Polisi nchini, Septemba 17 mwaka huu katika Shule ya Polisi Moshi (TPS).

**Babu amesema serikali ya mkoa huo pamoja na wadau wanaomuunga mkono, watatoa saruji hiyo ili kurejesha makazi hayo katika hali ya kawaida.**



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni ya Teknolojia na Mawasiliano ya Vodacom Tanzania, Jaji mstaafu Thomas Mihayo (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, baada ya mkutano mkuu wa mwaka wa wanahisa wa kampuni hiyo, Dar es Salaam mapema wiki hii. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Philip Besiimire (kushoto), Mjumbe wa Bodi ya wakurugenzi, Margaret Ikongo (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa Fedha, Hilda Bujiku. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachukua hatua kunusuru vyanzo vya maji

**Na Godfrey Mushi,** MONDULI

WADAU wa mazingira kutoka ndani na nje ya nchi, wameanza kuchukua hatua za makusudi kunusuru vyanzo vya maji vilivyoko hatarini kukauka katika misitu ya asili ya Serela na Losimingori iliyoko Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha.

Vyanzo hivyo ambavyo ndivyo tegemeo la maji yanayotumiwa na baadhi ya Tarafa za Wilaya hiyo, vimeharibiwa vibaya kutokana na ukataji hovyo wa miti ya asili, kwa ajili ya biashara ya kuuza kuni na ujenzi wa makazi ya jamii za kifugaji za Kimasai.

Kutokana na uharibifu huo, Mkurugenzi wa Shirika la Masai Pastoralist Development Organization (MPDO Lareto) linalofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Baraka Laizer, alisema wamelazimika kuwapelekea wakazi wa Kata za Serela na Repruko, mradi wa ufugaji wa nyuki kama chagizo la kiuchumi ili kuacha ukataji miti ndani ya misitu hiyo.

"Tangu tumebuni na kuuleta mradi huu wa ufugaji nyuki katika maeneo haya, wananchi wameacha kufanya uharibifu kwenye misitu ya asili ya Serela na Losimingori.

"Dhamira yetu ni kunusuru mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika eneo hili lenye vyanzo vya maji. Kwa ujumla mradi huu unalenga kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji; ambapo kwa sasa tunafanya kazi ya kuzijengea uwezo kamati zinazoshiriki kutunza mazingira na kulinda vyanzo hivi kwenye vijjji husika," alisema

Awali, Mratibu wa Mradi huo unaotekelezwa na MPDO Lareto, Amani Sekino, alisema kwenye mradi huo tayari zaidi ya wanawake 60 wamepatiwa mradi wa ufugaji wa nyuki na wameanza kunufaika kiuchumi.

"Wanawake wa jamii za kifugaji walio wengi, wanategemea kuendesha maisha yao kwa kukata miti ya misitu hii. Kwa hiyo, ili kuwapa motisha ya kuachana na uharibu wa misitu ya Serela na Losimingori na kuvinusuru vyanzo vya maji kutoweka, ndio maana tukaja na mradi huu wa kiuchumi," alieleza Sekino.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo kutoka Kikundi cha Enywata maa, Nalembo Ole Shulu, Mkazi wa Monduli, akieleza namna ulivyoanza kubadili maisha yao kiuchumi, alisema mradi huo umewasaidia kuwa chanzo cha kipato kutokana na kuuza mazao ya nyuki.

"Tunapata bidhaa nyingi za nyuki, ambazo ni tofauti na kurina asali kama tulivyozoea Watanzania." alisema.

Kitaalamu, nyuki huzalisha bidhaa nyingi ambazo zina faida kubwa kiafya pamoja na maendeleo ya kiuchumi, kama vile nta, sumu ya nyuki, maziwa ya nyuki, vumbi, supu yake na gundi.

Alipohojiwa na Nipashe kuhusu mchango wa serikali, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Isaac Joseph, alisema Halmashauri yao inaunga mkono ujio wa mradi huo, kwa kuwa ni mkombozi wa mazingira yaliyoharibiwa kwa ufekaji wa misitu kwenye baadhi ya vijjji, ili kuvuna miti ya ujenzi na biashara ya kuni.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA



# Majina ya utani ya wachezaji, Bruce Lee, Ninja, OCD yalivyotamba kwenye soka

**Na Adam Fungamwango**

TUNAONA siku hizi wachezaji mbalimbali wa timu za Ligi Kuu wakipewa majina na watangazaji wa redio na televisheni, mambo haya yalikuwepo tangu zamani.

Tofauti ni kwamba kwa sasa ni wachezaji wachache tu wenye majina ya utani au wanayopewa kwenye soka tofauti na zamani ambapo asilimia kubwa walikuwa na majina hayo ya utani.

Labda inawezekana kwa sababu sasa wachezaji wenye uwezo mkubwa wa vipaji na kupambana uwanjani si wengi kama ilivyokuwa huko nyuma.

Zamani wachezaji wengi walikuwa ni wapambanaji, hivyo wakapata majina kutokana na kufanana na kazi wanayoifanya uwanjani.

Hata wale waliokuwa na uwezo na vipaji, nao walipewa majina kutokana na jinsi walivyo.

Majina hayo yalitolewa na watu tofauti, kama siyo na watangazaji mpira, basi ni mashabiki wa soka.

Ilipendeza sana kumsikia mtangazaji walimtangaza mchezaji na kumtaja kwa jina lake alilopewa.

Na yalikuwa yakiwakaa vema kiasi kwamba huwezi kulitaja jina lake tu bila kutaja lile la utani.

Idd Pazi, golikipa wa zamani wa Simba na Taifa Stars yeye alipewa jina la 'Father' na wachezaji wenzake kwa heshima kubwa waliokuwa nayo kwake, pamoja na uwezo wake. Hadi leo hii, hata mchezaji ambaye ni staa kwenye timu basi anaitwa kwa jina hilo.

Zamoyoni Mogella yeye aliitwa 'Golden Boy', alilopewa na kocha Mjerumani Rudi Gutendorf aliyeifundisha Taifa Stars mwaka 1981, wakati huyo akiwa straika chupukizi wa Tumbaku ya Morogoro kabla ya kuhamia Simba mwaka huo huo.

Alikuwa akifunga bao kila akiingia dakika 20 za mwisho kwenye michuano ya Kombe la Challenge, kocha kaamua kumwita 'mwana wa dhahabu'.

Kulikuwa na beki mmoja wa kulia wa Simba anaitwa Daudi Salum, yeye alipachikwa jina la Bruce Lee kutokana na staili yake ya kuruka juu kwa ajili kupambana na mawinga hatari, akaitwa jina hilo la mfalme wa kung fu duniani.

Mohamed Kajole, beki wa kushoto wa Simba, yeye akapachikwa jina la Machela kutokana na aina yake ya uchezaji usio na mzaha, ulisababisha mawinga wengi kuumia na kupandishwa kwenye machela kwenda kutibiwa mara kwa mara nje ya uwanja.

Beki wa kati wa Tukuyu Stars na Yanga, Salum Kabunda anapewa jina la Ninja, kutokana na aina yake ya kupenda kutumia nguvu zaidi kwenye ukabaji wake, wakati mwingine akiruka miguu miwili. Aina hii ya uchezaji ndiyo anayo Abdallah Shaibu ambaye akapewa jina hilo hilo.

Said Swedi, straika wa Yanga yeye alipewa jina la 'Scud' kwani aliifunga Simba mara mbili kipindi ambacho kulikuwa na vita ya Ghuba mwaka 1990 hadi 1991, na ni makombora yaliyotumiwa sana na Iraq dhidi ya Marekani na washirika wake.

Kuna mchezaji wa Coastal Union, aliitwa Razack Yusuph, yeye aliitwa 'Careca', ambalo ni jina mchezaji nyota wa Brazil wakati huo.

Said Mwamba akapachikwa jina la Kizota, ambalo ni Jengo Bunge kwa wakati huo,

Wengine ni Celestine Mbunga 'Sikinde', Jose Ayoub 'Kwasakwasa, Frank Kasanga 'Bwalya', Ally Malilo 'Loketo', George Lucas 'Gazza', Aboubakar Salum 'Sure Boy, Deo Njohole 'OCD', David Mwakalebela 'MP', Mohamed Yahaya 'Tostao', Mohamed Bakari 'Tall', na Hamisi Gaga 'Gagarino.'

Wengine ni Idd Selemani 'Meya', Haruna Moshi 'Boban', Michael Paul 'Nylon', Peter Lupokela 'Gari Kubwa', John Makelele 'Ziga Zig', Malota Soma 'Ball Juggler', Samli Ayoub 'Beki Msaarabu', Mohamed Hussen 'Mmachinga', Itutu Kigi 'Road 'Master', Abbas Dilunga 'Sungura', Kitwana Manara 'Popat', na Makumbi Juma 'Homa ya Jiji'.

Pan African ilikuwa na beki mmoja wa kati akiitwa Rashid Idd, akipewa jina la Chama, lakini pia Yanga ilikuwa na beki wake wa kati akiitwa Athumani Juma ambaye naye akapachikwa jina la Chama. Simba nayo baada ya miaka kadhaa ikapata mchezaji mmoja aliyeitwa Athumani Jumapili, naye akaitwa 'Chama'.

**Beki wa kati wa Tukuyu Stars na Yanga, Salum Kabunda anapewa jina la Ninja, kutokana na aina yake ya kupenda kutumia nguvu zaidi kwenye ukabaji wake, wakati mwingine akiruka miguu miwili. Aina hii ya uchezaji ndiyo anayo Abdallah Shaibu ambaye akapewa jina hilo hilo.**

Hili jina lilikuwa maarufu sana nchini miaka ya 1980 hadi 1990, ambalo lilitokana na beki mmoja wa kati ya timu mbalimbali za Zambia na timu ya taifa, Dick Chama, miaka ya 1960 hadi 1970 aliyejipatia sifa kubwa kubwa kutokana na umahiri wake wa kupambana na mastraika wakorofi, ndiyo maana mabeki wengi vijana wakati huo wakajiita Chama.

Alikuwepo pia Boi Idd 'Wikens', Juma Pondamali 'Mensah' ambalo ni la kipa matata wa zamani wa Ghana, Robert Mensah.

Silvatus Ibrahim akaitwa Polisi, James Tungaraza 'Bolizozo' ambalo ni la mchezaji Jean Bolizozo wa Stella Abidjan aliyeifunga bao la pili kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho mwaka 1993, ikilala mabao 2-0. Jina hilo akapewa mchezaji huyo wa Yanga.

Wengine ni Methord Mogella 'Fundi', Sanifu Lazaro 'Tingisha', Godwin Aswile 'Scania', Yusuph Macho 'Musso', Twaha Hamudu Noriega, Juma Mkambi 'Jenerali', Rajab Rashid 'Msingida', Bakari Malima 'Jembe Ulaya', Sunday Manara 'Computer', Salum Mwinyimkuu 'Carlos', Ally Yusuph 'Tigana', Elius Michael 'Nyoka Mweusi', George Kulagwa 'Best', Said Maulidi 'SMG', Mahmood Nyalusi 'Shilton', Ezekiel Grayson 'Jujuman', Mao Mkami 'Ball Dancer', Steven Mapunda 'Garincha', Omari Hussein Keegan', Maalim Salehe 'Romario', Abdul Ramadhani 'Mashine', na Ishaka Hassan 'Chukwu', ambalo ni jina la beki wa zamani wa timu ya taifa ya Nigeri Christian Chukwu.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Trump akataa mdahalo mwingine na Kamala

**WASHINGTON,** MAREKANI

MGOMBEA wa chama cha Republican, Donald Trump, amekataa kushiriki mdahalo mwingine na Kamala Harris, wa chama cha Democrat kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu Novemba 5, mwaka huu.

Trump, alisema hawezi kushiriki mdahalo mwingine baada ya ule uliofanyika wiki hii Philadelphia kwa sababu aliibuka mshindi wa wazi.

Baada ya mdahalo huo, kura nyingi za maoni zilionesha wapiga kura walihisi kuwa Harris alikuwa amefanya vyema zaidi kuliko mpinzani wake Trump.

Rais huyo wa zamani aliongeza kuwa kusitishwa kwa mdahalo huo itampa nafasi Harris kufanya kazi yake kama makamu wa rais.

"Mshindi anaposhindwa katika pambano, maneno ya kwanza kutoka kinywani mwake ni nataka mechi ya marudiano. Kura za maoni zinaonesha wazi kwamba nilishinda mdahalo dhidi ya Kamala Harris, mgombeaji wa chama cha Democratic mwenye itikadi kali...na mara moja akaitisha mjadala wa pili," aliandika Trump katika ukurasa wake wa X.

**Baada ya mdahalo huo, kura nyingi za maoni zilionesha wapiga kura walihisi kuwa Harris alikuwa amefanya vyema zaidi kuliko mpinzani wake Trump.**

Hata hivyo, muda mfupi baada ya kauli hiyo, Harris akihutubia wafuasi wake katika jimbo la North Carolina, alijibu kwa kusema wapiga kura wanadai mjadala mwingine kwa sababu wanachopigania ni jambo muhimu.

Kura za maoni zilionesha kuwa wagombea hao wawili wako kwenye kinyang'anyiro kigumu ikiwa imesalia miezi miwili kabla ya uchaguzi.

Wote wawili walidai kupata ushindi baada ya mdahalo huo wa Jumanne uliochukua muda wa dakika 90 na kurushwa na kituo cha televisheni cha ABC News.

Katika mjadala huo, Harris alimkemea Trump kwa kumlenga na mashambulizi binafsi ambayo yalimfanya kujitetea.

Trump na wafuasi wake tangu wakati huo wamekuwa wakiwashutumu wanahabari wawili wa ABC ambao walisimamia mjadala huo kwa kutokuwa na haki na kumpendelea Harris.

**BBC**



Watu wakiwa katika uwanja wa shule ya Al-Jawni iliyoko Nuseirat Ukanda wa Gaza ambayo ilishambuliwa na Israeli, juzi. **PICHA: AFP**

# Russia yaionya Nato,Marekani

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amezionya nchi za Magaharibi kuacha mpango wake wa kuruhusu makombora yao ya masafa marefu kutumiwa na Ukraine kuishambulia nchi yake.

Putin alisema kwamba jumuiya ya kujihami ya Nato iko katika hatari ya kuingia vitani na Russia ikiwa Ulaya na Marekani zitairuhusu Ukraine kushambulia eneo la nchi yake kwa kutumia makombora hayo yaliyotengenezwa na nchi za magharibi.

Rais Putin aliiambia runinga ya serikali kwamba ruhusa hiyo haitamaanisha chochote ila ushiriki wa moja kwa moja wa nchi za Nato, Marekani na Ulaya katika vita hivyo.

"Utakuwa ni ushiriki wao wa moja kwa moja na kwa kweli, hii inabadilisha kwa kiasi kikubwa kiini na asili ya mzozo." alisema

Aliongeza "Ikiwa ni hivyo, tutachukua maamuzi yanayolingana kulingana na vitisho ambavyo vitatolewa kwetu."

Katika hatua nyingine, Msemaji wa Ikulu ya Russia, Maria Zakharova alisema wizara ya Mambo ya Nje inashirikiana na idara ya usalama ya FSB kufanya tathmini ya shughuli za wanadiplomasia wa Uingereza.

Wizara hiyo ilitoa taarifa kuwa ubalozi wa Uingereza ulioko Moscow ulikuwa umevuka makubaliano ya kidiplomasia.

Msemaji Maria Zakharova alisema wizara ilikubaliana na FSB kufanya tathmini ya shughuli za wafanyakazi hao wa ubalozi.

"Ubalozi wa Uingereza kwa kiasi kikubwa umekiuka mipaka iliyowekwa na Mkataba wa Vienna," alisema na kuendelea kuushutumu ubalozi huo kwa kufanya vitendo vinavyolenga kusababisha madhara kwa raia wa Russia.

**BBC**

## Sheria mpya kuigawa serikali Afrika Kusini

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

SERIKALI ya muungano ya Afrika Kusini, inakabiliwa na mgogoro kufuatia hatua ya Rais Cyril Ramaphosa, kutia saini sheria mpya ya elimu.

Chama cha Democrat Alliance (DA) ambacho kinashiriki serikali hiyo kinapinga sheria hiyo mpya ambayo inaondoa matabaka katika uandikishaji watoto katika shule za msingi.

Kabla ya uchaguzi mkuu uliofanyika Mei, vyama hivyo vikuu ambavyo kwa sasa vinaunda serikali vilikuwa vikizozana kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Elimu ya Msingi (Bela).

Ingawa ANC na DA zinagawana madaraka, bado hakuna makubaliano kuhusu mabadiliko hayo. Kiongozi wa DA,John Steenhuisen alisema kwamba ikiwa utiaji saini utatekelezwa chama chake kitalazimika kuangalia chaguo lingine kuelekea mbele.

Kifungu ambacho kimeibua utata zaidi ni kile kinachohusu kuimarisha usimamizi wa serikali kuhusu lugha na sera za uandikishaji.

Kifungu hicho nyeti kinahusiana na ushirikiano na usawa wa rangi.

Serikali ya awali ya ANC ilisema kuwa lugha na vigezo vingine vya kuandikishwa vilikuwa vinatumika kuzuia wanafunzi wengi hasa Waafrika kuandikishwa shuleni.

Ingawa ubaguzi wa rangi umemalizika, bado mgawanyiko wa rangi unaendelea katika baadhi ya maeneo ya elimu.

Shule za awali za wazungu bado zilikuwa na vifaa bora zaidi kuliko zile zinazohudumia jamii ya watu weusi.

Lugha ya Kiafrikana haijatajwa katika sheria hiyo, lakini ANC inasema kuwa baadhi ya watoto wanatengwa shuleni ambako lugha ya Waafrikana walio wachache inatumika kama njia ya kufundishia. **BBC**

## Papa Francis amaliza ziara Asia Pasifiki

**ROMA,** VATICAN

KIONGOZI Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amemaliza ziara katika nchi za Asia Pasifiki, akiacha ujumbe wa uvumilivu kwa dini tofauti.

Papa Francis alizuru nchi ya Indonesia yenye idadi kubwa ya Waislamu duniani ikiwa na waumini milioni 242.

Ziara hiyo kwenye nchi nne za eneo hilo ilianza Septemba 2, ilikuwa ndefu zaidi na yenye changamoto kwa kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 87.

Papa Francis alitumia ziara yake kuhubiri vipaumbele vyake vya msingi ikiwemo msisitizo juu ya mazungumzo baina ya dini na tamaduni mbalimbali, kutunza mazingira na kuhimiza mambo ya kiroho . **DW**

# Mbaroni madai mauaji ya wakala fedha mtandaoni

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe, linawashikilia Fanuel Seth, maarufu Fanu (24) mkazi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako na Batista Ngosso (30) kwa tuhuma za mauaji ya mfanyabiashara Godfrey Ndambo (45) aliyefariki dunia Julai 20, mwaka huu, kwa kupingwa na kitu kizito kichwani.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Ally Kitumbi, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa.

Alisema Ndambo aliyekuwa mfanyabiashara wa wakala wa fedha, aliuawa akiwa anaingia nyumbani kwake na watuhumiwa kumpora Sh. milioni 47.

"Upelelezi wa kesi hiyo umeshakamilika na watuhumiwa hawa watapelekwa mahakamani ili hatua zingine za kisheria ziendelee," alisema Kitumbi.

Kamanda Kitumbi alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Njombe ambao wanajihusisha na vitendo vya uhalifu na ukatili wa kijinsia kuacha mara moja kwa kuwa jeshi hilo halitafumbia macho uhalifu wa aina yoyote.

Mmoja ya mkazi wa Njombe, Raphael Nsumba alisema matukio ya wizi yamekuwa mengi, hivyo Jeshi la Polisi linatakiwa kuimarisha ulinzi ili kupunguza uhalifu.

"Matukio yamekuwa mengi leo unasikia huku kesho kule, hivyo ni vizuri Jeshi la Polisi likaongeza ulinzi ili kupunguza uhalifu mkoani kwetu," alisema Nsumba.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (wan ne kulia), akigawa mitungi ya gesi 1,000 kwa wanawake wa mkoa huo, iliyotolewa na kampuni ya Lake Gas, juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yakusanya Tril. 1.8/- madini, mafuta

**Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepata Sh. trilioni 1.877 kutoka kwenye kampuni 44 na sekta za madini, mafuta na gesi ikiwa na tofauti ya kati ya malipo na mapato ya Sh. milioni 402.41 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema jana katika uzinduzi wa ripoti ya 14 ya Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Mavunde alisema kati ya kampuni hizo, 26 ni za madini; saba za gesi asilia na mafuta na 11 ni kampuni zinazotoa huduma katika sekta za madini, mafuta na gesi asilia.

Pia alisema kampuni zilionesha kuwa zililipa Sh.trilioni 1.878 serikalini, hivyo kuwapo na tofauti kati ya malipo na mapato ya Sh. milioni 402 sawa na asilimia 0.021 ya mapato yote yaliyoripotiwa na serikali.

Aidha, Mavunde alielekeza tofauti hiyo ya Sh. milioni 402 kufanyiwa uchambuzi wa kina ili kujua visababishi vilivyosababisha kutofautiana ili kamati izipatie kampuni na serikali ushauri wa nini kifanyike ili tofauti hizo zisiendelee kujitokeza kwenye malinganisho yatakayofuata.

Alisema pamoja na masuala mengine yaliyomo ripoti ya TEITI pia imeweka wazi taarifa mbalimbali ili kutekeleza matakwa ya viwango vya kimataifa vya EITI pamoja na sheria inayosimamia shughuli za TEITI nchini.

Mavunde alisema taarifa hizo ni pamoja na takwimu za uzalishaji na usafirishaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia (production and export data), takwimu za ajira katika sekta ya uziduaji, michango ya kampuni kwa jamii (CSR) na ushiriki wa wazawa katika sekta ya uziduaji ikijumuisha kutoa huduma kwenye kampuni za uziduaji.

Awali, Mwenyekiti wa TEITI, Ludovick Utouh, alisema lengo la uzinduzi wa ripoti hiyo ni kuweka wazi kwa ajili ya wananchi na wadau mbalimbali kutumia takwimu zilizomo kufanya mijadala ya kuboresha na kuongeza mchango wa sekta ya madini, mafuta na gesi asilia katika pato la taifa.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dk. David Mathayo, aliipongeza serikali kwa kutoa taarifa ya wazi ya ulinganisho wa mapato yatokanayo na sekta ya uziduaji na kutumia fursa hiyo kuwataka Watanzania waipitie na kuona sekta ya uziduaji inavyochangia kukuza uchumi wa nchi na kuwataka pia wananchi kutumia taarifa hii kushauri na kutoa maoni yao.

# Jela maisha kubaka mtoto

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, imemhukumu kifungo cha maisha jela, Gabriel Barakael (35), maarufu kama Mangi, mkazi wa Boko Wilaya ya Kibaha baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka na kumnajisi mtoto wa miaka saba, mwanafunzi wa darasa la kwanza.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi na Hakimu mkazi Mwandamizi Fahamu Kibona baada ya kusikilizwa na kukamilika kwa ushahidi kutoka pande zote mbili.

Akisoma hukumu hiyo mahakamani hapo, Hakimu Kibona alisema siku ya tukio, Juni 2, mwaka huu, mtoto huyo alimwomba bibi yake kwenda kuchota maji ili afue nguo zake na wakati anarudi kutoka kisimani, alikutana na mshtakiwa ambaye alimvutia kichakani.

Kwa mujibu wa hakimu huyo, mshtakiwa alimvua nguo na kumpaka mafuta mtoto huyo sehemu za siri kufanikisha tendo hilo huku akimtishia kumfanyika kitu kibaya iwapo angemweleza mtu yeyote kuhusiana na kilichotokea.

"Mtoto huyu katika ushahidi wake alidai kwamba baada ya kufanya tendo hilo, mtuhumiwa alitumia maji yale aliyochota na kunawa kisha kuondoka na kumwacha akiwa na michubuko na maumivu," alisema Hakimu Kibona.

Ilidaiwa mahakamani hapo kwamba wakati mtoto huyo akirejea nyumbani, bibi yake alisikia kelele za mjukuu wake na kumsogelea akamkuta damu zinamvuja na alipomwuliza, alimwambia kwamba amebakwa na Mangi.

Bila kuchelewa, bibi huyo alitoa taarifa kwa majirani na Mwenyekiti hatimaye mtuhumiwa kukamatwa huku mtoto akipelekwa hospitalini kwa uchunguzi na matibabu.

Taarifa kutoka katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani Tumbi, ilidai kuwa daktari alibaini michubuko kwa mtoto huyo, nguo kuwa na matone ya damu huku akiwa hana tena bikra baada ya kubakwa.

Upande wa mashtaka, Mawakili wa Serikali Neema Kwai na Asifiwe Mnzava waliwasilisha mashahidi sita wakiwamo bibi wa mtoto huyo, baba, mgambo, daktari, askari mpelelezi na mtoto mwenyewe huku upande wa utetezi akiwapo mshitakiwa na kaka yake.

Hakimu Kibona alisema upande wa utetezi, mshitakiwa alijitetea kwamba wana ugomvi na bibi wa mtoto huyo baada ya kaka yake kumshtaki ndugu wa bibi anayejulikana kwa jina la Masanja kwa mwenyekiti kwa madai ya kuiba mahindi.

Hata hivyo, Hakimu Kibona alisema mahakama imeridhika na ushahidi kutoka upande wa mashtaka hasa mwathirika mwenyewe ambaye alieleza namna mshtakiwa alivyomwingilia kwa kumpaka mafuta sehemu za siri na ushahidi wa bibi na daktari aliyefanya uchunguzi.

Hakimu alisema sababu za ugomvi wa wizi wa mahindi si za msingi na utetezi huo bali ulikuwa namna ya kuihadaa mahakama.

Kifungu 130 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Na. 16 ya mwaka 2022 kinakataza dhana nzima ya kosa la kubaka na mazingira yake.

Kutokana na hukumu hiyo, Hakimu Kibona alisisitiza vifungu hivyo vimetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kumlinda mtoto na kuhakikisha anapata haki yake. Alisema haki hizo zimo kwenye Katiba ya ya Jamhuri ya Tanzania na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia kuhakikisha haki zote hazivunjwi.

HADITHI

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-30

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Pamoja na kwamba yeye hakuwa na ujuzi wa upelelezi, lakini kila alipoirudisha akili yake nyuma, akagundua kuwa hakuwa mwendawazimu wa kawaida.

"Du! Yule hakuwa mwendawazimu. Yule ndiyo mpelelezi aliyekuwa anawawinda walinzi ili waingie ofisini mwangu kuchukua flashi. Hapo ndipo Materu alipogundua kuwa suala lile ni kubwa kuliko mwenyewe alivyodhani.

Ni kwamba watu walikuja na kuwapiga walinzi wa jengo lile, hawakuiba kitu chochote kile, ila walichukua flashi zake mbili ambazo zina mambo yake ya siri ambayo kama yakiwekwa hadharani, siyo tu kwamba hatogombea tena ubunge, bali hata anaweza kwenda kutundikwa kitanzini. Miguu ilimtetemeka na kujihisi kabisa yupo hatarini. Alijua kabisa kuwa flashi zile zimechukuliwa kwa sababu ya kwenda kuzitoa hadharani ili kumuumbua.

Kitu ambacho kilimtia wasiwasi zaidi ni kwamba hakujua ni lini au wakati gani ambapo watu hao watafanya kazi hiyo ya kuziweka hadharani, watatumia njia gani na mbaya zaidi hakujua ni kina nani, licha ya juhudi kubwa ya kutumia pesa nyingi kutaka kuzuia chochote kitakachoonekana kinataka kumtia doa.

Mambo yote hayo, yalimyima usingizi kabisa na kuwa na wasiwasi mkubwa licha ya utajiri alionao.

Mpaka sasa ni yeye pekee aliyekuwa anajua sababu ya watu wale kuvamia jengo hilo. Wakati wengine wakiwa mshangao kuwa wamefanya hivyo bila kuchukua chochote, yeye anafahamu kuwa lengo lilikuwa ni kutwaa zile flashi mbili.

******************************

Wasiwasi wao haukuwa wa uongo. Kila kitu kilichofanyika kilifanywa na Afande Willy pamoja na Kamal mwenyewe.

Afande Willy alipendezwa sana na Kamal. Uwezo wake wa kiakili na mambo anayoyowaza na kuyafanya, yalimfurahisha na kweli kama alivyoambiwa na kaka yake Dokta Shija, yalifanana sana na askari wapelelezi.

Mara kwa mara baada ya kurejea kazini walifanya wote mazoezi uani, kwani afande Willy, alikuwa amenunua.

Alimwambia kuwa hakutakiwa kuwa fundi gereji, bali askari polisi tena mpelelezi. Alipoambiwa historia yake kuwa alikuwa akipenda sana kusoma vitabu vya kipelelezi, pamoja na filamu zake, hakushangaa.



**Afande Willy alipendezwa sana na Kamal. Uwezo wake wa kiakili na mambo anayoyowaza na kuyafanya, yalimfurahisha na kweli kama alivyoambiwa na kaka yake Dokta Shija, yalifanana sana na askari wapelelezi.**

"Kwa umri ulionao bado hujachelewa sana rafiki yangu." Mara kwa mara afande huyo huwa anamwambia, lakini Kamal huona kama anapewa moyo tu.

"Sasa rafiki yangu nataka nikupime kama wewe kweli unaweza kazi ya upelelezi." "Kwa vipi afande?" Akauliza Kamal siku moja baada ya kumaliza mazoezi na kukaa mezani wakila supu, mikate na mayai ya kuchemsha. "Kuna kazi ngumu kidogo nataka kuifanye, lakini kwa sababu nimekuangalia nimeona wewe utaiweza. Kama ingekuwa mwingine wala nisingemtumbukiza kwenye janga."

"Vyovyote vile mimi niko tayari kunipa misheni ya kwenda kuifanya." Akajibu Kamal. Afande Willy akacheka. "Hii ni kwa ajili ya wewe rafiki yangu. Kumbuka tunaifanya kazi hii kwa kujipa mamlaka sisi wenyewe. Tunafanya hivi kwa sababu siyo kukuokoa wewe ili asiende kuning'inizwa kitanzini kwa tuhuma za kumuua mpenzi wako Mariamu kimakosa, lakini pia kuuweka ukweli hadharani ambao umefichwa kwa sababu ya rushwa. Kwetu nchini rushwa ni adui wa haki. Lakini wenye pesa wamepenyeza pesa kuanzia hospitalini hadi kwenye Jeshi la Polisi kwa wale ambao si waaminifu ambao wamewaaminisha wananchi uongo. Wamewaaminisha mashetani wame malaika na malaika kuwa mashetani." Akaongea Afande Willy kwa uchungu. Kabla Kamal hajaongea lolote akaendelea. "Nataka hata kama nikipata adhabu kwa kufanya kazi ambayo sikutumwa, lakini wananchi watambue ukweli wa hili upo wapi. Naweza kuhukumiwa na jeshi langu, lakini si na wananchi." "Mhh! Umeanza lini kuwa mwanasiasa?" Kamal aliuliza kwa utani, kabla ya wote wawili kuangua kicheko. Baada ya hapo mipango ikaendelea. Afande Willy akamkumbusha kuwa kaka yake Dokta Shija ameshakusanya baadhi ya vielelezo ambavyo wanaweza kuvitumia kwa ajili ya kumuweka kadharani kinara ya mauaji, hivyo Kamal naye akatumwa kazi ya kuifanya mahali ili kukamilisha ushahidi.

"Kuwa makini, nakuamini Kamal, najua wewe si askari, lakini ifanye kama afande kwa sababu umekaa kama afande na mbinu zote ulizozifanya kuwakimbia askari wasikukamate hata mimi nimekuvulia kofia, ndiyo maana nimekuamini." "Kwa sababu umesema niko kama afande, mimi ndiyo mhusika ambaye anatuhumiwa na mauaji, na namsaka muuaji wa mpenzi wangu, ambaye amenigeuzia kibao. Nitaifanya kazi hii kwa umaridadi mkubwa na hutaamini." Afande Willy alicheka, akampa mkono. Wakashikana mikono ishara kuwa wamekubaliana na hicho kitakachokwenda kufanyika. Na ndicho kilichofanyika.

Plani ilipangwa na afande Willy, ikatekelezwa na wote wawili na mafanikio makubwa. Siku mbili nzima Kamal alikuwa akikusanya vitu ambavyo alidhani anaweza kuvaa na kumfanya awe mwendawazimu kamili.

Baada ya kuhakikisha amekusanya chupa, makopo na viroba, alichukua na kupitia magazeti ya zamani aliyoyahifadhi yenye picha za wendawazimu kadhaa halisi.

Aliangalia kwa muda na kuvutiwa na staili moja ya uvaaji wa mwendawazimu. Akaamua hiyo ndiyo ataitumia.

Akaanza kazi ya kuunganisha makopo, chupa, viroba na vitu vingine ambavyo aliona vinafaa kwa kazi hiyo.

Pamoja na kwamba ilionekana anakwenda kufanya kufanya kazi ya hatari, lakini moyoni mwake alikuwa na furaja sana kwa sababu tatu. Kwanza atakuwa anaifanya kazi ambayo itakuwa ni kisasi cha wote waliomuua mpenzi wake. Pili ni kujiokoa mwenyewe kwenye kitanzi cha mauti, kwani anatafutwa na kesi ya mauaji ya huyo huyo mpenzi wake. Tatu ni kwamba aliuhusudu sana kazi ya upelelezi, ingawa hakuiweza kuipata na kuifanya, lakini amekuwa akiishi na damu hiyo na leo hii amepata fursa hiyo tena kutoka na askari polisi aliyempa kazi hiyo, ambaye ndiyo mtu pekee aliyeamua kujitolea kumsaidia kutoka kwenye janga la kusingiziwa mauaji.

Baada ya kuridhika usiku wa kwanza alifanya majaribio na kupita kwenye jengo la ofisi hizo.

Afande Willy alimwambia anachotakiwa kukifanya ni kuingia ndani ya jengo hilo, ghorofa ya pili, chumba namba 12, ambamo ndimo zilizomo ofisi za Materu. Afande huyo alisema kutokana na intelejensia yake inaonyesha kuwa ndani humo, kuna droo ambayo ina siri zote za mazungumzo pamoja na bbaadhi ya picha za video za mauji ya Mariamu.

Hivyo akamwambia anatakiwa kuingia humo kwa hila. Na hawezi kuingia kabla ya kukabiliana na walinzi wanaolinda hapo ambao wana silaha nzito. Kuingia kwa kuvamia ndani ya ofisi ya Materu haiwezekani kiusalama kwani wanafanya kazi ambao Jeshi la Polisi haiitambui.

Kwa maana hiyo wanatengeneza mpango wa Kamal kujifanya mwendawazimu anayepita hapo mara kwa mara ili kuwapumbaza walinzi watakiwe naye makini kabla ya kuwavamia. Kamal alipewa bastola na daktari Shija kaka yake afande Willy, kwani afande huyo hakutaka kutoa ya kwake. Lakini Willy akamsisitizia kuwa aitumie pale tu itakapolazimika na aamini sana nguvu zake za mwili.

*Itaendelea Jumamosi*

HABARI MICHEZO

## Aomba kura tuzo za TMA

**Na Christina Haule, Morogoro**

MSANII wa muziki wa Taarabu kutoka Morogoro, Amina Kidevu, amesema ana nafasi ya kushinda tuzo za Muziki Tanzania ,Tanzania Music Award' (TMA) kama atapigiwa kura na Wananchi.

Msanii huyo ameteuliwa kuwania tuzo katika vipengele viwili vya muimbaji bora wa kike pamoja na wimbo bora wa mwaka, tuzo hizo zimepangwa kufanyika Septemba 29.


Amina, alisema hiyo ni mara yake ya kwanza kuchaguliwa kushiriki katika tuzo hizo na ameona muda umefika wa yeye kufanya hivyo sababu ni mwimbaji wa muda mrefu.

Alisema ameamua kujaza fomu na kutuma wimbo wake alioimba wa ,Hatuachani' na ,Utakalo halikuwa' ambapo wimbo uliopita ni Hatuachani.

Aidha, Amina aliwaomba watanzania kumpigia kura kupitia namba maalum ya T 2605 na T 2802 ili kuweza kushinda katika vipengele hivyo.

"Naomba mnipigie kura nipate kushinda, mimi ni malkia wa Morogoro lakini natamani siku moja nije niwe malkia wa Tanzania nzima, nitakapopata tuzo nitapata nguvu kubwa kufanya mengi katika tasnia yangu ya sanaa" alisema Amina.

Alisema katika vipengele hivyo kwenye kinyang'anyiro hicho atawania tuzo na wasanii Leyla Rashid, Mwinyimkuu kutoka Zanzibar, Salha Abdalah na Mwasiti.



# MSHAMBULIAJI DODOMA JIJI FC AWEKA REKODI

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI Paul Peter wa Dodoma Jiji, juzi aliweka rekodi ya kufunga bao la mapema zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, alipopachika bao sekunde ya 39 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara timu yake ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo.

Akiwa ndani ya eneo la hatari, aliupata mpira ambao uliokolewa na mabeki wa Namungo ndani ya eneo hilo, akawahadaa na kupiga shuti kwa mguu wa kulia uliotinga wavuni likiwa bao pekee katika mchezo huo.

Katika mabao 30 ya Ligi Kuu yaliyofungwa mpaka jana, bao hilo ndilo linakuwa bao la mapema zaidi mpaka sasa tangu kuanza kwa msimu huu.

Mechi hiyo ilichezwa Uwanja wa Tanzanine Kwaraa, Babati, Manyara, ambapo Dodoma Jiji imeuchagua kuwa uwanja wake wa nyumbani kwa muda kutokana na kufungiwa kwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mecky Maxime, alisema wameshinda mchezo huo kwa bahati kwani walikuwa na makosa mengi sana ambayo kama wapinzani wao wangekuwa makini wangewaadhibu.

"Mchezao wa leo tulikuwa na bahati tu ya kushinda, dakika 25 za mwisho gemu ikatuponyoka, ikawa siyo ya kwetu, tukawa hatuna utulivu, tunapoteza mipira mingi hasa eneo letu la hatari, wao wenyewe Namungo hawakutulia, lakini tunashukuru kwa kupata pointi tatu na hii ni ligi, ushindi wa leo utatusaidia kuona wapi tunaelekea," alisema kocha huyo.

Naye Kocha wa Namungo, Mwiyi Zahera, alilalamikia safu yake ya ushambuliaji kukosa nafasi kadhaa mabazo zilipaswa kuwa mabao.

"Wapinzani wetu walifanya makosa mawili au matatu ya wazi ambayo tulitakiwa kufunga, hiki ndicho kilichosababisha tufungwe leo, hatuna umaliziaji mzuri eneo la mwisho, wenzetu wamepata nafasi chache sana, nadhani mbili tu, moja wameitumia," alisema Zahera.

Hiki ni kipigo cha tatu mfululizo kwa Namungo tangu kuanza kwa ligi kwani awalai ilifungwa na mabao 2-1 na Tabora United na baadae kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Fountain Gate, kabla ya juzi kukutana na kipigo hicho cha bao 1-0.




Gwiji wa soka Afrika, Nwankwo Kanu (kushoto) akipokea jezi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Philip Besiimire ikiwa ishara ya kuunga mkono ziara ya mbio za Baiskeli za ,Twende Butiama 2024' kupitia taasisi yake ya Kanu Heart Foundation. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# 100 kushiriki mbio za baiskeli za 'Twende Butiama' 2024

**Na Shufaa Lyimo**

WASHIRIKI zaidi ya 100 wamethibitisha kushiriki mbio za kuendesha baiskeli za kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa Julius Nyerere.

Mbio hizo za kila mwaka zilizopewa jina la ,Twende Butiama', zitafanyika mapema mwezi ujao na kilele chake kuwa Oktoba 14 siku ya maadhimisho ya kifo cha baba wa taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Kampeni za mbio hizo, Gabriel Landa, alisema lengo la hizo ni kumuenzi Mwalimu Nyerere kwani alikuwa anapenda kutumia usafiri huo.

"Kampeni ya msafara wa Twende Butiama ina lengo la kumuenzi Mwalimu Nyerere vile vile tunatambua ukiendesha baiskeli unajenga afya ndio maana kampeni hii inahamasisha Wananchi kujenga afya pamoja na kutunza mazingira kwa kuwa tunatambua maeneo endelevu hutegemea mazingira," alisema Landa.

Mwenyekiti huyo alisema msafara huo utatumia baiskeli kwa umbali wa kilomita 1500, na kudai watazunguka mikoa 12 ya Tanzania Bara, ambapo watatoa madawati zaidi ya 1000, watapanda miti 6000 pamoja na kujenga kambi za afya kwenye mikoa ambayo msafara huo wa waendesha baiskeri utapita.

Aliwataka watanzania watumie usafiri wa baiskeli kwani husaidia kujenga afya pamoja na kujikinga na mgonjwa yasiyoambukiza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mahusiano na Mawasiliano wa Kampuni ya Vodacom, Zuwena Farah alisema lengo la kuingia ubia na Kampeni hiyo ni kuboresha elimu, afya pamoja na kutunza mazingira na kupitia kambi kambi za afya na kutoa msaada.

"Tumeingia ubia na Kampeni hii ya Twende Butiama kwa lengo la kutoa elimu ya afya na mazingira kwa wanafunzi ili wawe na utamaduni wa kuyatunza," alisema Zuwena.

## ZISIKUPITE

### EZE ATAKIWA MAN UNITED
MANCHESTER United inamfuatilia winga wa Crystal Palace, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 26 na huenda ikamtafuta mshambuliaji huyo wa England msimu ujao. ***(Manchester Evening News)***

### LIVERPOOL PIA WANAMTAKA
LIVERPOOL inaweza pia kumnunua Eberechi Eze ikiwa fowadi wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32, hatasaini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(Liverpool Echo)***

### FOFANA ATAKIWA ATHENS
CHELSEA inatarajia kumuuza mshambuliaji wa Ivory Coast, David Datro Fofana mwenye umri wa miaka 21, kwa klabu ya Ugiriki ya AEK Athens. Dirisha la uhamisho la Ugiriki lipo wazi hadi leo Jumatano.***(The Athletic)***

### POCHETTINO ATAJWA MAREKANI
KOCHA wa zamani wa Chelsea na Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino anatarajiwa kuthibitishwa kuwa kocha mpya wa Marekani baada ya kukutana na wakuu wa soka wa nchi hiyo. ***(Mail)***

### ANTONY KUACHIWA KWA MKOPO
KLABU ya Manchester United ina nia ya kumuachia winga wa Brazil Antony kwa mkopo huku Fenerbahce ikiwa katika nafasi nzuri ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.***(Sun)***

### DAVIES AWANIWA GALATASARAY
KLABU ya Galatasaray ina nia ya kumsajili beki wa Tottenham Hotspur na Wales, Ben Davies mwenye umri wa miaka 31 kabla ya dirisha la uhamisho la Uturuki kufungwa Septemba 13. ***(Football Insider)***

### OBI ALIMSHAWISHI OSIMHEN
KIUNGO wa kati wa zamani wa Chelsea, John Obi Mikel alijaribu kumshawishi mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, kujiunga na The Blues kabla ya uhamisho wake wa mkopo kutoka Napoli kwenda Galatasaray majira ya kiangazi. ***(Talksport)***

### RAMOS KUTUA CORINTHIANS
MLINZI wa zamani wa Real Madrid na Hispania, Sergio Ramos huenda akakaribia kujiunga na klabu ya Brazil ya Corinthians. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38 amekuwa hana klabu tangu alipoondoka Sevilla majira ya joto. ***(Itatiaia)***

### RABIOT KIZUNGUMKUTI UNITED
MAHITAJI ya mshahara ya kiungo Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29 ni makubwa mno kwa Manchester United kumsajili Mfaransa huyo, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Juventus. ***(Football Insider)***

### JUVE YAMUWEKA SOKONI MELO
KLABU ya Juventus bado iko tayari kupokea ofa kwa kiungo wa kati wa Brazil, Arthur Melo mwenye umri wa miaka 28 ambaye anataka kusalia na kupigania nafasi yake katika klabu hiyo. ***(Fabrizio Romano)***

### JONATHAN DAVID AITAKA EPL
MSHAMBULIAJI wa Canda, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24, yuko kwenye mazungumzo kuhusu mkataba mpya na Lille lakini anaendelea kuhusishwa na kuhamia Ligi Kuu ya England, EPL. ***(Teamtalk)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LAMINE YAMAL AKATAA KULINGANISHWA NA MESSI

Amesema anataka kuwa na uchezaji wake na kulinganishwa na Muargentina huyo ni....

**BARCELONA, Hispania**

NYOTA wa Barcelona na Hispania, Lamine Yamal amesema anataka kuwa na uchezaji wake mwenyewe na kwamba kulinganishwa na Lionel Messi sio haki kwani haiwezekani kufikia kiwango hicho.

Yamal tayari alikuwa kwenye rada za ulimwengu wa soka kutokana na nafasi yake pale Barcelona katika umri mdogo na akawa mfungaji mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya LaLiga Oktoba mwaka jana, lakini wasifu wake ulikuzwa zaidi msimu huu wa majira ya joto baada ya kuisaidia Hispania kutwaa taji la Ulaya.

Kando na kuwa nyota aliyechipukia katika michuano hiyo nchini Ujerumani, pia aliweka alama mpya kwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kushiriki Euro alipoingia uwanjani dhidi ya Croatia katika hatua ya makundi.

"Ninapenda wananifananishe na mchezaji bora zaidi katika historia ya soka, lakini nataka kuwa mimi mwenyewe," alisema Yamal akikiambia kituo cha televisheni cha Hispania, Antena 3 alipoulizwa kuhusu kufananishwa na mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Argentina. „Kufikia kiwango cha Messi haiwezekani."

Alioneshwa kwenye picha ya 2007 akiwa na Messi wakati akiwa na umri wa miezi sita tu, akionekana na nyota huyo wa zamani wa Barcelona katika kalenda ya hisani baada ya kushinda shindano.

"Jamani, alipitisha baadhi ya nguvu zake kwangu," Yamal alisema. „Bado nina mengi ya kutoa."

Fowadi huyo chipukizi alifunga bao zuri la kusawazisha katika mechi ya nusu fainali ya Euro dhidi ya Ufaransa na kuweka kikosi kilichopata ushindi fainali dhidi ya England.

Baada ya fainali hizo, Transfermarkt ilimthamini kwa tahamni ya kufikia euro milioni 120.

# TEN HAG AMJIBU CRISTIANO RONALDO



**MANCHESTER,** ENGLAND

KOCHA Erik ten Hag amemjibu Cristiano Ronaldo kwa kusema fowadi huyo wa Ureno hajui anachozungumzia kwa sababu yuko „mbali na Manchester.“

Ronaldo alimkosoa Ten Hag katika mahojiano na Rio Ferdinand kwa kusema kocha huyo wa United hapaswi „kusema kwamba hutapigana kushinda ligi au Ligi ya Mabingwa Ulaya.“

Ten Hag, amepuuza maoni hayo huku akisisitiza ni Ronaldo aliyesema United haiwezi kushinda taji la Ligi Kuu.

„Alisema kwamba Manchester United haiwezi kushinda Ligi Kuu, namshangaa,“ alisema Ten Hag, ambaye alikosana na Ronaldo wakati wakiwa pamoja kwenye klabu hiyo.

„Alisema hivi. Ukisoma makala vizuri sana. Yuko mbali sana nchini Saudia mbali na Manchester kwa hiyo kila mtu anaweza kuwa na maoni na ana haki ya kuwa na maoni. Ni sawa.“

Ten Hag yuko kwenye presha kabla ya safari ya kuelekea Southampton leo Jumamosi kufuatia kichapo cha 3-0 kutoka kwa Liverpool kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

Mkurugenzi Mtendaji, Omar Berrada na mkurugenzi wa michezo Dan Ashworth wote wamemuunga mkono hadharani Mholanzi huyo.

Lakini hilo halijazuia uvumi kwamba kocha huyo wa zamani wa Ajax anaweza kutimuliwa Old Trafford miezi michache tu baada ya mkataba wake kuongezwa hadi 2026.

„Haina athari kwangu,“ alisema Ten Hag. “Najua katika mchakato huu tulipo, tunakwenda wapi, tupo kwenye kipindi cha mpito, tunatakiwa kuwaunganisha wachezaji wengi chipukizi kwenye timu.

„Lazima turudishe wachezaji majeruhi kwenye timu. Kabla ya mtu yeyote kufikiria visingizio, tunapaswa kushinda kila mchezo, najua hilo. Timu inajua hili. Tutazingatia kila mchezo na kuwa na mawazo

# PSG yaamuliwa imlipe Mbappé euro Mil 55

**PARIS,** UFARANSA




TUME ya Sheria ya Ligi Kuu ya Ufaransa imeiamuru PSG kumlipa Kylian Mbappé euro milioni 55 ikiwa ni malimbikizo ya mshahara ambayo hajalipwa, kwa mujibu wa ESPN.

Tume hiyo ilithibitisha uamuzi huo kwa waandishi wa habari bila maelezo zaidi, siku moja baada ya nyota huyo wa Ufaransa kukataa ofa ya upatanishi ya tume katika mzozo wake na klabu yake hiyo ya zamani.

Maofisa wa PSG na wawakilishi wa Mbappé walikutana mjini Paris siku ya Jumatano baada ya Mbappé kuitaka tume kuhusika.

Mbappé alijiunga na Real Madrid msimu huu wa majira ya joto kwa uhamisho wa bure.

Baada ya mkutano huo, wawakilishi wa Mbappé waliiambia AP kwamba mshambuliaji huyo aliiomba tume kuzingatia kutolipwa kwa mishahara wa miezi mitatu na theluthi ya mwisho ya bonasi ya uaminifu.

PSG haina nia ya kulipa na ilitangaza kuwa itachukua hatua zaidi za kisheria.

“Kwa kuzingatia mapungufu ya wigo wa kisheria wa tume kuchukua uamuzi kamili juu ya suala hili, suala hilo sasa lazima lipingwe katika kongamano lingine la kisheria, ambalo PSG inafurahi kuwasilisha ukweli wote katika miezi na mwaka ujao,“ klabu ilisema katika ujumbe wake kwa AP.

“Kama suala la sheria na ukweli, mchezaji ameweka wazi, mara kwa mara ahadi za umma na za kibinafsi ambazo lazima ziheshimiwe, baada ya kupewa faida ambazo hazijawahi kufanywa na klabu kwa miaka saba huko Paris,“ PSG ilisema baada ya tangazo la tume.

“Na klabu inatazamia haya kusimamiwa katika chombo kinachofaa, ikiwa mchezaji anataka kufuatilia suala hili la uharibifu usioeleweka zaidi, kwa wakati unaofaa.“

Uhusiano wa Mbappé na PSG ulimalizika huku kukiwa na mvutano mkubwa wakati wa msimu wake wa mwisho katika klabu hiyo.

# Rodri: Kushinda Ballon d'Or itakuwa ndoto iliyotimia

**MANCHESTER,** ENGLAND

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Rodri ameiambia ESPN itakuwa „ndoto iliyotimia kwangu“ kushinda Ballon d'Or na kumaliza miaka 64 ya Hispania ya kungoja mshindi wa wanaume baada ya kuibuka mpinzani mkubwa wa Vinícius Júnior katika tuzo za mwaka huu.

Rodri mwenye umri wa miaka 28, anatajwa kuwa na nafasi kubwa nyuma ya fowadi huyo wa Real Madrid kushinda Ballon d'Or baada ya kuisaidia City kunyakua taji la nne mfululizo la Ligi Kuu England msimu uliopita kabla ya kutangazwa kuwa Mchezaji Bora wa Euro 2024 baada ya kuisaidia Hispania kutwaa ubingwa msimu huu. .

Licha ya kushinda mataji mfululizo ya Euro 2008 na 2012 na kubeba Kombe la Dunia la 2010, hakuna Mhispania aliyeshinda Ballon d'Or tangu kiungo wa zamani wa Barcelona na Inter Milan, Luis Suarez mwaka 1960.


Lakini akizungumza na ESPN, Rodri anasema kuwa itakuwa fahari kwake na kwa Hispania kushinda Ballon d'Or itakapotolewa huko Paris Oktoba 28.

“Ndio, bila shaka itakuwa ndoto kwangu,“ alisema Rodri.

„Kuna watu wengi ambao wanasema ikiwa Rodri atashinda, ni vipi, kwa mfano, Andrés Iniesta au Xavi hawakushinda?

“Kwa kiasi fulani, nakubali. Walikuwa wachezaji ambao waliashiria enzi, na walikuwa bora zaidi katika historia, lakini pia ni kweli kwamba, siku ya mwisho, walikuwa sehemu ya kizazi ambacho kilijumuisha Lionel Messi na Cristiano.

„Lakini itakuwa ni fahari kwangu na kwa nchi yangu kushinda. Kuwa na mwakilishi wa Hispania ambaye ana uwezo wa kushinda Ballon d'Or kunaboresha kila mtu.“



HABARI MICHEZO

# MWAMUZI, MKUFUNZI MSTAAFU ABDULKADIR AFARIKI DUNIA

**Na Mwandishi Wetu**

MWAMUZI na Mkufunzi wa waamuzi mstaafu wa FIFA, Omar Abdulkadir amefariki dunia juzi na kuzikwa jana katika makaburi ya Kisutu, Dar es Salaam.

Abdulkadir ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Chama cha Waamuzi Taifa (FRAT), hadi anafikwa na umauti juzi alikuwa amelazwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) akipatiwa matibabu ya maradhi ya kisukari kwa muda mrefu.

Msiba uko nyumbani kwake maeneo ya Mtoni kwa-Aziz Ally, Temeke, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, mtoto wa marehemu, Ahmed Abdulkadir alisema baba yake ameugua kwa muda mrefu maradhi hayo na kupelekea akatwe mguu chini karibu na kifundo mwaka jana.

Abdulkadir ambaye alizaliwa mwaka 1959, ameacha mke mmoja na watoto sita.

Wakati huo huo Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia ametuma salamu za pole kwa ndugu, jamaa na familia ya mpira wa miguu kufuatia kifo cha mwamuzi huyo.

Karia alisema mchango wa Abdulkadir katika maendeleo ya mpira wa miguu kwenye eneo la waamuzi hapa nchini utakumbukwa daima.



Mchezaji wa timu ya Kitunda FC, Adebi Ali (jezi ya bluu), akiwania mpira wa juu na mchezaji wa Mipango FC, Mwita Samwel, kwenye mchezo wa kirafiki katika Uwanja wa Kitunda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Viongozi TWFA kujulikana leo

**Na Mwandishi Wetu, Moshi**

VIONGOZI watakaoongoza Chama cha Mpira wa Miguu Wanawake wanatarajiwa kujulikana leo kwenye uchaguzi wa chama hicho unaofanyika Mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi huo, Benjamin Kalume alisema wanaowania nafasi ya Mwenyekiti wa TWFA ni Somoe Ng'itu na Amina Karuma.

Pia alisema katika nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) inatakiwa mmoja na wapo Zena Chande ambaye anatetea nafasi yake na Fatuma Seleman na Veronica Samo.

Kadhalika katika nafasi ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji wanaonia ni Irene Ishengoma, Ndinagwe Sungura na Mwanaheri Kalolo na wanaotakiwa ni wawili tu.

„Maandalizi yote yamekamilika, wajumbe na wagombea wote wamewasili Moshi na wengine tunatarajia watafika jioni ya leo (jana)" alisema Kalume.

Kalume alisema watakaochaguliwa watakaa madarakani kwa muda wa miaka minne na jumla ya wajumbe wa mkutano wanaotakiwa kupiga kura ni 52 kila mkoa ukiwakilishwa na wajumbe wawili.

## Gamondi atamba kuonesha ukubwa

INATOKA UK. 24

na mchezo mgumu.

"Siyo mechi rahisi na hasa ukicheza michuano ya kimataifa, kila timu ni ngumu, ina kiwango kikubwa na ni mabingwa kwenye nchi yao, lakini tunataka kufanya kila njia ili kuwadhibiti wapinzani wetu kwenye mchezo wa kwanza. Nataka tusipoteze, tupate matokeo mawili, ushindi au sare ili iwe mechi rahisi nyumbani," alisema kocha huyo ambaye msimu uliopita aliifikisha timu hiyo hatua ya robo fainali.

Gamondi alisema hakupata chochote cha kumsaidia kwa wachezaji wa CBE ambao walikuwa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Ethiopia kilichocheza dhidi ya timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Septemba 4, hivyo maandalizi yake yametokana na taarifa za mchezo ambazo timu hiyo ilicheza dhidi ya SC Villa ya Uganda.

"Sikupata kitu chochote ambacho kinaweza kunisaidia kuwasoma wapinzani, kwa sababu wachezaji wao wanne wote hawakucheza, walikaa benchi tu, na pia hata kama wangecheza mfumo wa uchezaji wao timu ya taifa ungekuwa si sawa na wanapocheza kwenye kikosi cha CBE, hivyo isingenisaidia sana," alisema Gamondi.

Yanga ilitinga raundi ya kwanza ikishinda mabao 10-0 dhidi ya Vital'O ya Burundi, ikishinda mabao 4-0 mchezo wa kwanza na 6-0 mchezo wa pili, michezo yote ikipigwa, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

CBE ilifanikiwa kutinga hatua hiyo kwa kuifunga SC Villa nchini Uganda mabao 2-1 na kutoka sare ya bao 1-1 nyumbani.

Baada ya mechi ya leo, mchezo wa marudiano unatarajiwa kuchezwa Septemba 20 na mshindi wa jumla atatinga hatua ya makundi ya ligi hiyo.

## Fei Toto: Samatta bado muhimu

INATOKA UK. 24

inatokea tu kushinda ugenini na nyumbani kushindwa," alisema mchezaji huyo.

Alisema kwa sasa akili zao wanazielekeza kwenye maandalizi kujiandaa na michezo miwili dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo itakayochezwa Oktoba 7 nchini DR Congo na Oktoba 15, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Stars inashika nafasi yapilikwenye msimamo wa kundi lao baada ya kukusanya pointi nne katika michezo miwili wakifuatiwa na Ethiopia wenye pointi moja huku Guinea wakiburuza mkia kwa kutokuwa na pointi.

Congo inaongoza kundi hilo kwa kuwa na pointi sita huku kila timu ikiwa imecheza michezo miwili.

# Michezo

Jumamosi Septemba 14, 2024

Nipashe

## Yamal akataa kulinganishwa na Messi

UKURASA 21





Wachezaji wa Yanga, Dickson Job (kulia) na Clement Mzize (kushoto) wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo jana kwenye uwanja wa Abebe Bikila, Adis Ababa, Ethiopia kujiandaa na mchezo wa leo wa ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya kwanza dhidi ya CBE ya nchini humo, anayeonekana kwa mbali ni beki, Ibrahim Bacca. **PICHA: MTANDAO**

# Gamondi atamba kuonesha ukubwa

### Ni katika mchezo wa leo ugenini, ingawa ameonesha....

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, leo saa 9:00 alasiri kwa saa za Tanzania wanatarajiwa kushuka kwenye Uwanja wa Abebe Bikila, Addis Ababa, nchini Ethiopia kucheza na mabigwa wa nchi hiyo CBE katika mchezo wa mkondo wa kwanza, raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Kocha Miguel Gamondi akiahidi kuonesha ukubwa wao, licha ya kukiri kuwa hautokuwa mchezo rahisi kama wengi wanavyodhani.

Akizungumza kutoka nchini humo, Gamondi amesema CBE, inayomilikiwa na Benki ya taifa ya nchi hiyo, ni ngumu na ni mabingwa wa Ethiopia hivyo anatarajia mchezo mgumu ingawa ni lazima Yanga waoneshe ukubwa wao.

„Katika mchezo wa leo tunawaheshimu wapinzani wetu, tupo ugenini, lakini kwa timu kubwa kama Yanga tunatakiwa kuonesha ukubwa wetu, tuwe na nguvu ya kukabiliana nao," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Alisema amekuwa akiwasikia watu wakiibeza timu hiyo na kudhani mechi itakuwa rahisi kwa timu yake, lakini haitokuwa hivyo, na ndiyo maana amewaandaa wachezaji wake kukabiliana

INAENDELEA UK. 23

# Fei Toto: Samatta bado muhimu sana Taifa Stars

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Feisal Salum ‚Feitoto' amesema kuwa mshambuliaji Mbwana Samatta aliyetangaza kupumzika kuichezea timu hiyo bado anahitajika na muhimu kwenye kikosi chao.

Akizungumza juzi baada ya kurejea nchini akitokea Ivory Coast, ambako Stars ilicheza mchezo wa pili wa Kundi H dhidi ya Guinea, kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zitakazofanyika mwakani nchini Morocco, Fei Toto, alisema hawezi kuingilia mawazo ya mtu au maoni yake, lakini Samatta bado anahitajika kwenye kikosi hicho kwani angewasaidia kwenye harakati za kusaka tiketi, lakini pia ni kiongozi mzuri nje na ndani ya uwanja.

"Huwezi kuingilia mawazo au maoni ya mtu, inawezekana mwenyewe kakaa na watu wake wamemshauri hivyo, lakini pamoja na hayo bado naona anahitajika sana, sisi pia tunamhitaji kwenye kikosi chetu kwa sababu ni mchezaji mzuri na amekuwa na mchango mkubwa kwenye kikosi cha Taifa Stars, ni nahodha wetu na wachezaji tunampenda, amekuwa akituongoza vizuri ndani na nje ya uwanja, ila sasa sujui mwenyewe kama anaweza kubadili au kuendelea na msimamo wake, huwezi kumuingilia," alisema Fei Toto.

Akizungumzia ushindi wa mchezo wa ugenini dhidi ya Guinea, alisema baada ya sare dhidi ya Ethiopia walikaa wao wachezaji na benchi la ufundi na kuamua kwenda kusaka ushindi ugenini kwa udi na uvumba na kweli wakafanikiwa.

Kuhusu Stars kutoshinda nyumbani na kufanya vyema ugenini, Fei Toto alisema huwa inatokea tu na wala siyo kwamba wanapanga au kuna kitu ndani yake.

„Mpira una matokeo matatu, kushinda, sare na kufungwa, sisi kila mchezo tunataka kushinda, huwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002